


**WAKUU wa Nchi kuridhia mpango upatikanaji nishati barani Afrika**
UKURASA 5

**KIKWETE akoshwa maendeleo visiwani, asema Zanzibar ya zamani si ya sasa**
UKURASA 17

**GACHAGUA ahoji kugeuzwa mbuzi wa kafara Kenya**
UKURASA 19

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

**OLMO ATABAKI BARCELONA - FLICK**
UKURASA 22

Jumatatu Januari 6, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581914
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Heche akoleza moto CHADEMA



John Heche

**AJITOSA** kumvaa Wenje; aweka wazi kumuunga mkono Lissu, atanguliza onyo kwa wajumbe wa Kamati Kuu... *Ukurasa wa 2*

**UBADHIRIFU TISHIO...**

## DED awakaribisha wananchi wamhoji matumizi ya fedha

UKURASA 2

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77/- | Bil 770.91/- | Bil 676.66/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/- | Bil 297.86/- | Bil 499.96/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36/- | Bil 2,015.78/- | Bil 1,234.67/- |
| Jumla | Bil 1,770.84/- | Bil 4,590.73/- | Bil 3,084,55/- | Bil 2,411.29/- |

*Mwenendo wa viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23. CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya taasisi ya WAJIBU. Uk. 4*

UKURASA WA 24

## KIUNGO SIMBA ATIMKIA ULAYA

KIUNGO mshambuliaji aliyekuwa akifuatiliwa kwa karibu ili kujiunga na Klabu ya Simba kipindi hiki cha dirisha

## Mwingine atoweka, gari lake lakutwa limetelekezwa, polisi watoa neno

UKURASA 18

**MICHEZO** **RAMOVIC: HII NDIYO YANGA NILIYOTAKA** UK. 24 **KATUNI** UK. 6



Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi akimsikiliza Profesa Bernadeta Killian akitoa maelezo ya kitaalamu ya ujenzi wa jengo la taaluma na utawala la Taasisi ya Sayansi za Bahari la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, linalojengwa katika eneo la chuo hicho, Buyu Wilaya ya Magharibi "B" Unguja. **PICHA: IKULU**

# DED akaribisha wananchi wamhoji matumizi ya fedha

**Na Joseph Mwendapole**

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Khamis Katimba amewataka wananchi kufika ofisini kwake kuhoji matumizi ya fedha zinazokusanywa na kutumika kwenye halmashauri hiyo.

Alitoa msimamo huo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza katika kikao cha wadau wa maendeleo katika ukumbi wa halmashauri hiyo huku akisisitiza kuwa kila fedha inayokusanywa na kutumika ina maelezo yake.

Katimba alitoa kauli hiyo baada ya Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Sebastian Waryuba ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kikao hicho, kumshauri kuwaeleza wananchi matumizi ya fedha zinazokusanywa na halmashauri hiyo.

Waryuba alianza kwa kumsifu mkurugenzi huyo kuongeza mapato na hata kukusanya asilimia 82 ya mapato ya ndani kwa miezi sita pekee (Julai - Desemba 2024).

"Nimefurahi kushuhudia kasi hii ya ukusanyaji mapato bila kutoana damu, mabadiliko haya yanaonesha kwamba huko tuendako tutafika salama.

"Mkurugenzi kasi hii isipungue, umeaminiwa na sisi tunakuamini kwa mikakati yako, simama imara na makusanyo yetu yapande zaidi lakini waone na matumizi yake," alisema Waryuba.

Akitoa ufafanuzi wa kauli hiyo ya Waryuba, Mkurugenzi Katimba alisema wananchi wakiona fedha zao zinafanya kazi gani, watahamasishana kulipa kodi kwa hiari.

"Mimi ninawaahidi, wao kazi yao ni kulipa kodi halafu waje wanawajibishe kwa matumizi ya fedha zao. Ninawaomba waendelee kulipa kodi ya serikali, lakini waje kuniwajibisha kwa matumizi ya fedha zao.

"Ofisi yangu ipo wazi kwa wote, hata akija mmoja mmoja ninaruhusu aje ofisini kwangu, aje aniulize 'umekusanya shilingi ngapi na umetumia shilingi ngapi?' Nitamueleza. Ofisi ipo wazi, ni ofisi ya wananchi wote, sisi ni dhamana tu," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Pius Mwelase alisema halmashauri hiyo ilikuwa haijawahi kukusanya mapato ya ndani asilimia 82 katika kipindi cha miezi sita pekee.

"Haijawahi kutokea mpaka Desemba kukusanya asilimia 82 kwenye halmashauri yetu, viporo vyote toka halmashauri yetu ianze tunavimaliza na kama kuna vingine semeni, sasa pesa ipo.

"Ubunifu aliokuja nao mkurugenzi wetu umeleta mabadiliko makubwa mno, tunajivunia na tunaamini bado tuna muda wa kutosha wa kukusanya fedha zingine nyingi kutokana na mikakati iliyopo kwa sasa," alisema.

Akizungumza mwenendo wa makusanyo katika wasilisho lake, Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, Richard Sanga alisema kuwa mpaka kukamilika kwa mwaka wa fedha 2023/24, halmashauri hiyo ilikusudia kukusanya Sh. bilioni 22.338 lakini ilifanikiwa kukusanya Sh. bilioni 20.445.

Alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2024/25, halmashauri hiyo iliidhinisha Sh. bilioni 26.790, mapato ya ndani yakiwa ni Sh. bilioni 4.334 na mpaka sasa - kwa miezi sita - mapato ya ndani, zimekusanywa Sh. bilioni 3.567.

Wakizungumza kwenye mjadala wa Rasimu ya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Halmashauri hiyo kwa kipindi cha 2025/26, wadau wamegusia maeneo kadhaa wakitaka yafanyiwe kazi.

Mwananchi Omari Jumanne alisema halmashauri inapaswa kuandaa mpango madhubuti kuhakikisha wafugaji wanafuga kisasa na kuachana na ufugaji wa samaki wa kizamani.

"Samaki wanalipa hapa kwetu Malinyi, halmashauri isaidie sasa namna ya ufugaji kisasa, hili litasaidia kuongeza mapato," alisema.

Mwananchi mwingine Milard Ngapulile alishauri halmashauri kuandaa mfumo mzuri wa motisha kwa walimu na hata kulipa walimu wanaojitolea.

"Halmashauri itenge fedha kwa ajili ya walimu wanaojitolea na si kuwaachia mzigo huo walimu wakuu. Pia halmashauri inapaswa kuongeza motisha kwa walimu," alisema.

Neema Mgalagala alishauri kuwapo minada ya nyama choma ili wananchi wakajiliwaze baada ya kutafuta pesa.

"Tunatafuta fedha lakini hakuna pa kuzitumia, kwanini na sisi tusiwe na mnada wa mbuzi tukajipumzishe, tunahitaji kujiliwaza kwa kula vitu vizuri," alisema.

Rai ya mkurugenzi huyo kukaribisha wananchi kufuatilia matumizi ya kodi zao (makusanyo ya serikali) utaongeza uwajibikaji katika fedha za umma nchini ikiwa kutakuwa na mwamko huo kwa wananchi, pia wakurugenzi wengine kuruhusu wananchi kujua matumizi ya kodi zao.

Taarifa rasmi za kiserikali zinaonesha kupotea mabilioni ya shilingi ambayo yangetumika kuboresha miundombinu nchini.

Mtazamo huo wa fedha za umma kufanyiwa ubadhirifu, hata kusababisha pengo la ufanisi kwenye huduma za umma, unawasilishwa kupitia Uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2022/23 uliofanywa na taasisi ya WAJIBU.

Taasisi hiyo inayosimamiwa na CAG mstaafu Ludovick Utouh, mwanazuoni wa uhasibu, imebaini miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu wa fedha za umma, inayofikia Sh. trilioni 11.857 ndani ya miaka minne (2019/20 - 2022/23).

Kiasi hicho kama kingeelekezwa kutatua uhaba wa miundombinu shuleni, kwa mfano, kingetosha kujenga vyumba vya madarasa mapya 592,850.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), chumba kimoja cha darasa kinajengwa kwa Sh. milioni 20 kikiwa na samani zake zote.

| Taasisi | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 |
|---|---|---|---|---|
| Serikali Kuu | Bil 560.19/- | Bil 1,781.77/- | Bil 770.91/- | Bil 676.66/- |
| S/Mitaa | Bil 863.85/- | Bil 1,400.6/- | Bil 297.86/- | Bil 499.96/- |
| Mashirika | Bil 346.8/- | Bil 1,408.36/- | Bil 2,015.78/- | Bil 1,234.67/- |
| Jumla | Bil 1,770.84/- | Bil 4,590.73/- | Bil 3,084,55/- | Bil 2,411.29 |

Mwenendo wa viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu kuanzia mwaka 2019/20 hadi 2022/23. **CHANZO: Ripoti ya Uwajibikaji ya taasisi ya WAJIBU. Uk. 4**

# Heche akoleza moto CHADEMA

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Heche amekoleza moto katika mnyukano unaoendelea wa wanachama na wafuasi wa chama hicho.

Hii ni baada ya kuchukua na kurejesha fomu ya kuwania nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Taifa huku akiweka wazi kuwa anamuunga mkono Tundu Lissu katika mbio za kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa.

Vilevile, Heche aliyewahi kuwa Mbunge wa Tarime kwa tiketi ya CHADEMA, pia amewataka wajumbe wa Kamati Kuu kusikiliza alichokiita "sauti za wanachama".

Heche alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, wanachama na waandishi wa habari kuhusu nia yake ya kuwania nafasi hiyo. Aliwataka wajumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA kuhakikisha wanasikiliza sauti ya wanachama na kufanya uamuzi sahihi bila kufuata mahitaji yao binafsi wakati wa uchaguzi wa viongozi wakuu wa chama hicho mwezi huu.

"Mkienda na matamanio yenu na kusikiliza vichwa vyenu na matumbo yenu, wanachama hawatowaelewa miaka yote," Heche aliwaonya.

Alisema kuwa katika kuwania uongozi ndani ya chama hicho, yeye anamuunga mkono Lissu, mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti Taifa kutokana na mrengo wake wa kutaka haki, ukweli na uwazi ndani ya chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Heche alisema 'Kambi ya Lissu' wana uhakika wa kuchukua kiti na kuongoza chama hicho na kuwa hawako tayari kuona kinaongozwa na malengo ya watu binafsi kinyume cha madhumuni ya kuanzishwa kwake.

"Chama hiki kimeanzishwa kwa madhumuni maalumu ikiwa ni pamoja na kushinda dola na kuiondoa CCM (Chama Cha Mapinduzi), kulinda na kutumia rasilimali za nchi kwa manufaa ya watanzania, kuwapatia huduma bora watanzania ikiwa ni pamoja na matibabu, elimu na umiliki wa rasilimali binafsi," Heche alisema.

Alisema kuwa watu wengi wamefariki dunia kwa namna tofauti katika kuhakikisha wanapigania maslahi ya chama hicho, hivyo hawako tayari kuona kinaongozwa kwa malengo binafsi.

**UCHAGUZI MKUU**

Kuhusu chama hicho kushiriki Uchaguzi Mkuu mwaka huu, Heche alisema wakipata nafasi hiyo hawatakubali kushiriki bila kuwa na mabadiliko ya Tume ya Uchaguzi.

"Tutapeleka nguvu ya umma na tuna imani watasimama na sisi kama walivyosimama nasi katika mabadiliko mbalimbali kuhakikisha tunashinikiza serikali kufanya mabadiliko ya Tume ya Uchaguzi kabla ya Uchaguzi Mkuu na tutasimama katika msimamo wetu kuwa 'no reform no election' (hakuna mabadiliko hakuna uchaguzi," alisema Heche.

**KUKICHAFUA CHAMA**

Kuhusu madai kwamba Lissu anachafua chama, Heche alisema anaunga mkono kampeni za Lissu kuwasema na kuibua kashfa za baadhi ya watu wanaodaiwa kupokea rushwa ndani ya chama hicho.

"Kuna watu wanachafua viongozi wengine, wanamwita Lissu muongo, si kweli! Lissu ni mkweli na mtu safi. Yeye anachokifanya ni kuwavua nguo wanaovua nguo chama na wala si chama chenyewe.

"Wananchi wakikwambia wanataka mchicha ukawaletea vitu vingine kwa madai zote ni mboga za majani, hawatokuelewa," alisema Heche.

Heche pia alisema anamheshimu Mwenyekiti wa sasa, Freeman Mbowe kama baba yake na mlezi wa kisiasa na kuwa haitotokea kumkosea heshima. Anao mchango mkubwa katika demokrasia ya taifa na chama chao.

Baadhi ya wananchi mkoani Mwanza, akiwamo Anthelius Audax walisema kuwa kwa sasa chama hicho kimekua, hivyo viongozi wake wanahitaji kuwa makini ili kuhakikisha wanamaliza uchaguzi wao wa ndani bila kuwa na mvurugano ambao utasababisha mpasuko.

Wakati dirisha la kuchukua fomu ya kuwania uongozi ndani ya chama hicho kitaifa likifungwa jana, John Heche anakuwa mshindani wa pili katika nafasi ya Makamu Mwenyekiti, akitanguliwa na Ezekia Wenje aliyechukua na kurejesha fomu Januari 3 mwaka huu.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## MIAKA 61 YA MAPINDUZI

# Dk. Mwinyi ajivunia maendeleo katika elimu na uchumi wa bluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema Zanzibar imepata maendeleo kila sekta, ikiwamo ya elimu katika miaka 61 ya mapinduzi.

Alisema hayo wakati akiweka jiwe la msingi jengo la utawala na taaluma katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Taasisi ya Sayansi za Bahari huko Buyu, nje ya mji wa Zanzibar.

Rais Dk. Mwinyi alisema sera kuu ya uchumi katika serikali yake ni uchumi wa buluu na katika sekta hilo kuna utalii ambao unachangia pato la taifa kwa asilimia 30.

Alitaja sekta zingime ni uvuvi, kilimo cha mwani na mazao ya baharini, hivyo chuo hicho ni muhimu na nchi itapata wataalam wa uvuvi na mazao ya bahari.

Alisema sekta nyingine ni bandari, mafuta na gesi, usafiri na uzalishaji baharini, hivyo taasisi ya chuo hicho ni muhimu na itatoa wataalam wa uchumi wa buluu.

Rais Dk. Mwinyi alisema matarajio kuwa chuo kitatumia utafiti mbalimbali wa uchumi wa buluu na wataalam watakaotoka hapo wataleta utafiti huo na kusaidia kupata maendeleo.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Jakaya Kikwete alisema kuwa bila uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia mradi wa HIT unaofandhiliwa na Benki ya Dunia, shughuli hiyo isingefanyika na kwa uamuzi huo anastahili kupongezwa kwa kuwa haikuwa rahisi kushajiisha taasisi hiyo kwenye mradi huo.

Alisema isingeweza kufanya ujenzi huo bila kuwa na hatimiliki ya ardhi ya eneo la chuo hicho ambayo ni moja ya masharti ya Benki ya Dunia na kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kukipatia chuo hati hatimiliki ya ardhi katika eneo hilo na kukamilisha ujenzi wa barabara katika eneo hilo.

Kikwete, Rais wa Tanzania wa Awamu ya Nne, alisema hatua hiyo imerahisisha usafiri kwa wanafunzi na wafanyakazi na kusema kuwa Dk. Mwinyi hana mbadala wake katika utekelezaji ahadi zake za maendeleo.

Alisema kasi ya maendeleo Zanzibar ni kubwa na maendeleo yanafanyika. Zanzibar ya zamani si sawa na ya sasa.

Waziri wa Uchumi wa Buluu, Shabani Othman alisema kwenye sera ya uchumi wa buluu, kuna vipaumbele vitano, ikiwamo uvuvi na ukulima wa mwani ikijumuisha mazao ya baharini.

Alisema ili kutimiza malengo katika vipaumbele hivyo, kunahitajika rasilimali watu, utafiti na teknolojia na utalamu, vyote hivi sasa vipo katika chuo hicho, hivyo wizara yake itatoa ushirikiano kwa chuo.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema katika kufanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu, serikali imewekeza katika uchumi wa buluu na Zanzibar lazima izae matunda. Wizara yake imeandaa mitaala ambayo itatoa wanafunzi wenye sifa watakaojiunga katika chuo hicho.




Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi akiondoa pazia kuweka jiwe la Msingi la Ufunguzi wa Shule ya Sekondari Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, ufunguzi huo ulifanyika juzi ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. PICHA: IKULU

**"Tunachofanya leo ni sehemu tu ya miradi ambapo Serikali ya Tanzania ilichukua mkopo Benki ya Dunia kuimarisha elimu ya chuo kikuu na taasisi za elimu ya juu Tanzania ili kutawanya fursa ya elimu ya juu," alisema.**

Alisema wizara itahakikisha inawajengea wanafunzi ujuzi wa ziada ili kutoa mabaharia wengi na watalamu wa uvuvi ambao watatumia vifaa vya kisasa katika kuvua.

Waziri wa Elimu na Sayansi, Prof. Adolf Mkenda, alisema bila mapinduzi, mageuzi ya elimu yasingeweza kufikiwa.

Alimpomgeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuhakikisha hakuna mkwamo katika ujenzi huo na kupongeza serikali kwa uamuzi wa kuazisha Chuo cha Teknolojia ya ICT na kampasi ya chuo hicho ya kimataifa kuazishwa Zanzibar.

"Tunachofanya leo ni sehemu tu ya miradi ambapo Serikali ya Tanzania ilichukua mkopo Benki ya Dunia kuimarisha elimu ya chuo kikuu na taasisi za elimu ya juu Tanzania ili kutawanya fursa ya elimu ya juu," alisema.

Waziri Mkenda alisema chuo hicho kimepata mgawo wa fedha hizo Sh. bilioni 34.6 na kuvitaka vyuo vikuu kutoa shahada zinazoendana na mageuzi ya elimu.

Akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu mradi huo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam, Prof. William Anangisye, alisema mradi huo ni uwekezaji unaofanyika kwa lengo la kuzalisha maarifa ya kuimarisha taaluma ndani na nje ya nchi kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

Alisema hiyo pia ni mkakati wa chuo kuzalisha maarifa, utafiti na kuimarisha mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi na wafanyakazi.

Alisema mradi huo unatekelezwa na serikali kupitia Wizara ya Sayansi na Teknolojia kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa lengo la kuimarisha elimu ya vyuo vikuu nchini, kikiwamo Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewapatia hekta 50.24 katika eneo la Buyu ambako ndiko kiliko chuo hicho. Ujenzi wa mradi huo ulianza mwaka 2022 na hadi kukamilika kwake utagharimu jumla ya Sh. bilioni 11.1 na utakamilika Agosti mwaka huu.

Alisema kuwa mradi huo utakapokamilika, utaleta mabadiliko makubwa ikiwamo kuongezeka kwa wanafunzi kutoka 140 hadi 300, kuongeza fursa ya kuambatanisha wanataaluma katika kampuni za kazi na kutembelewa na wanataaluma waliobobea ili kubadilishana uzoefu kwa wanafunzi, kuongeza ubora wa ufundishaji na ufunzaji na kuongeza soko la ajira kwa ujumla.

Alimpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa mafanikio makubwa katika miaka ya uongozi wake ambayo yamefanyika kwa ufanisi mkubwa na yamejionesha katika uimarishaji uchumi, miundombinu, ukusanyaji mapato na kusimamia matumizi ya fedha za umma.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA NJONBE, RUKWA, SONGWE NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NYASA, MBINGA, MJI WA MBINGA, WILAYA YA SONGEA NA MANISPAA YA SONGEA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na route ya tisa utafanyika katika Mikoa ya Njombe, Rukwa, songwe na Ruvuma katika Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji wa Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea tarehe 12 hadi 18 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumapili tarehe 12 hadi siku Jumamosi tarehe 18 Januari, 2025.
2. VITUO: Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 03 Januari, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**




Askari wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) Mkoa wa Songwe wakiwa kwenye mazoezi wakati wa kutoa zawadi kwa askari waliofanya vizuri katika kazi za kipolisi mkoani humo mwishoni mwa wiki. **PICHA:JESHI LA POLISI**

# 173 watiwa mbaroni, wamo wa tuhuma za mafuta ya transfoma kukaangia chipsi

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani limewakamata watuhumiwa 173 wa makosa mbalimbali, yakiwamo ya usafirishaji nyara za serikali, dawa za kulevya, pombe haramu na wizi wa mifugo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase amesema watuhumiwa hao walikamatwa katika msako uliofanyika mwezi Desemba 2024 kwa lengo la kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu katika mkoa huo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake mwishoni mwa wiki, Kamanda Morcase alisema kuwa katika msako huo, pia zilikamatwa nyaya za kopa Kg 3,687, mafuta ya diseli lita 3,547, mafuta ya transfoma lita 80 pombe ya moshi lita 86, bangi kilo tatu na gramu 120.5, mirungi Kg 7.04 na ng'ombe sita walioibwa.

Kuhusu nyaya za kopa, kamanda huyo alisema tayari watuhumiwa sita wamekamatwa huku wanne wengine wakishikiliwa na jeshi hilo wakihusishwa na lita 80 za mafuta ya transfoma zilizokamatwa.

Alisema ipo dhana imejengeka kuhusiana na mafuta ya transfoma kuwa ni mazito na yanapotumika kukaanga chipsi na samaki, hayaishi kwa haraka, jambo ambalo linachangia kutokoma wizi wa mafuta hayo.

**"Mafuta haya yanadaiwa kutumika kukaangia chipsi au samaki kwa madai kwamba hayaishi haraka na ndio maana wanaendelea na wizi. Katika hili tunaahidi tutalikomesha, halitaendelea tena katika mkoa wetu," alionya.**

"Mafuta haya yanadaiwa kutumika kukaangia chipsi au samaki kwa madai kwamba hayaishi haraka na ndio maana wanaendelea na wizi. Katika hili tunaahidi tutalikomesha, halitaendelea tena katika mkoa wetu," alionya.

Kwa upande wa nyara za serikali, Kamanda Morcase alisema watuhumiwa wanne walikamatwa wakiwa na meno ya tembo manane yanayokadiriwa kuwa na uzito wa Kg 67, vichwa vitano na miguu 53 ya mnyamapori aliyefahamika kwa jina la tohe na nyama ya swala vipande vinane vyenye uzito wa Kg 32.

Kamanda huyo pia alisema kuwa katika kipindi cha mwezi Desemba, kesi 125 zilifikishwa mahakamani. Kati yake, 47 zilipata mafanikio na kesi mbili kati ya tano za ukatili wa kijinsia zilipata ushindi.

Kamanda Morcase alisema katika kesi hizo za ukatili wa kijinsia, mtuhumiwa mmoja aliyekutwa na hatia alifungwa kifungo cha maisha gerezani kwa kosa la kubaka na kulawiti na mwingine alihukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani kwa kosa la unyanyasaji kingono.

# Askari polisi waliong'ara kiutendaji wapewa zawadi

**Na Mwandishi Wetu,** SONGWE

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Augustino Senga ametoa zawadi kwa askari waliofanya vizuri katika kazi za polisi baada ya kukagua mazoezi yaliyoandaliwa na Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU) mkoani hapa.

Zawadi hizo ni pamoja na fedha taslimu zilizotolewa Januari 4 mwaka huu na kueleza kuwa kipekee ameanzisha utaratibu wa kutoa zawadi kwa askari wanaofanya vizuri katika mambo mbalimbali katika kazi za polisi.

Alisema lengo la kutoa zawadi ni kujenga uwezo zaidi na kutatua changamoto za jamii ili wananchi waendelee kuwa na imani na Jeshi la Polisi.

Alisema zawadi hizo pia zinalenga kutambua na kuthamini jitihada za askari wanaofanya vizuri, akiahidi kuwa zoezi hilo litakuwa endelevu mkoani humo.

Sambamba na hilo, Kamanda Senga alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan na Mkuu wa Jeshi la Polisi, IGP Camillus Wambura kwa kuendelea kutatua changamoto za jeshi hilo, hasa katika suala la rasilimaliwatu na vifaa.

## KUPOTEA KWA CHETI



**AGAPE COSMAS KAYOMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0692/0001** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ROSMINI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/2045/2025.**

## ANATAFUTWA



Pichani ni **Mzee Heshima Twaha** Heshima mwenye umri wa miaka 73 mkazi wa Makorora Mzingani Tanga anatafutwa na ndugu zake. Hajaonekana nyumbani tangu mwezi wa pili 2024 alipotoka kuelekea kwenye shughuli zake Arusha. Yeyote atakayemuona awasaliane nasi kwa simu namba 0653297730 au kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi imetolewa wa namba: **PHQ/TAN/TAN/44/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ABASI NASSORO** anatangaza kupotelewa na vyeti. Kidato cha nne index namba **S1241-0044 JUHUDI SECONDARY SCHOOL** mwaka **2006.** Cheti cha Chuo Ordinary Diploma **NTA 6** chenye Registration namba 20073101 cha **MBEYA INSTITUTE OF SCIENCE AND TECHNOLOGY (MIST)** mwaka **2010.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi. Taarifa za polisi: **PHQ/DAR/ILA/2342/2025, PHQ/DAR/ILA/2340/2025**

**IN THE DISTRICT COURT OF MBEYA**
**AT KYELA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 31971 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE:**
**JORAM NTONDOLO MWANGUPILI---------DECEASED**
**AND**
**In the matter of Application for letters of Administration by: JULIUS JORAM MWANGUPILI---------PETITIONER**

**(GENERAL CITATION (Rule 75)**


ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 16th day of January, 2025.

Dated at Morogoro this 19TH day of December 2024.




## KUBADILISHA JINA



Mwenye picha hapo juu anatangaza kubadilisha jina lake katika kitambulisho cha Taifa (NIDA) kutoka **YUNIKA EMMANUELY ABERD kwenda YUNIKA MOHAMEDI ABEID.**

Nazidi kusisitiza kwamba kuanzia leo hii mahali popote nitambulike kwa jina la **YUNIKA MOHAMEDI ABEID** badala ya **YUNIKA EMMANUELY ABERD.**



Muokota chupa tupu za plastiki akiwa kazini Mbezi Luis Dar es Salaam jana. Uwepo wa watu hawa umesaidia kukabiliana na uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji ovyo chupa hizo. **PICHA:SABATO KASIKA**

# Wakuu wa nchi Afrika kuridhia mpango mahususi wa nishati barani humo

**Na Elizabeth Zaya**

MKUTANO wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Nishati, unatarajiwa kuridhia, kusaini Mpango Mahsusi wa Nishati Afrika, kuidhinisha awamu ya kwanza ya Mipango ya Kitaifa ya Nishati kwa kipindi cha 2025 hadi 2030 na kupitisha tamko la Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Umeme na Nishati Mbadala wa Wizara ya Nishati, Innocent Luoga, mambo hayo makuu matatu yatafanyika katika mkutano huo utakaofanyika kati ya Januari 27 na 28, mwaka huu na yatasaidia kuweka ramani ya kimkakati kwa maendeleo ya nishati barani Afrika yenye lengo la kukuza upatikanaji wa nishati endelevu na ya haki kwa wote. Kadhalika, alisema nchi 14, ikiwamo Tanzania, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Nigeria, Zambia na Senegal, zitashiriki katika mpango huo wa kina wa kuboresha upatikanaji wa nishati na uhakika wa umeme katika maeneo yao.

Kwa upande wa tamko la Dar es Salaam, alisema litasaidia kuainisha maono ya pamoja ya Afrika kuhusu maendeleo ya nishati endelevu na kuwa mwongozo wa kuendeleza nishati mbadala, kuboresha miundombinu na kuhakikisha usawa wa upatikanaji wa nishati barani kote.

Alisema mkutano huo unalenga kuleta pamoja marais wa Afrika na wadau kuhamasisha mabadiliko katika sekta ya nishati Afrika na kwamba watu 1,500 wanatarajiwa kushiriki.

Luoga, alisema mkakati wa nchi hizo kwa sasa ni kuja na mpango mahsusi ujulikanao kama 'mission 300' unaolenga kuweka mkazo kuharakisha matumizi ya nishati safi, endelevu na nafuu kwa watu milioni 300 Afrika ifikapo mwaka 2030.

Alisema mpango huo unalenga kupunguza pengo la upatikanaji wa umeme barani humo kwa kupanua miundombinu ya nishati katika maeneo ambayo hayajafikiwa.

Akizungumza wakati wa kufungua warsha ya waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Gerson Msigwa, Msemaji Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema fahari ya Tanzania ni kuwa mwenyeji wa mkutano huo.

Msigwa, alisisitiza jukumu la Tanzania kama kiongozi wa kuendeleza nishati mbadala Afrika.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake wa kimkakati katika kuendeleza miradi ya nishati safi na kulifanya taifa kuwa mstari wa mbele kupigania nishati safi ya kupikia na suluhisho endelevu la umeme.

Alibainisha kuwa juhudi za kidiplomasia za Rais Samia zimeiweka Tanzania katika nafasi ya kipekee katika mazungumzo ya nishati Afrika.

"Tunaheshimika kuwa kitovu cha mijadala hii muhimu, huku mkutano huu ukiashiria hatua kubwa kuelekea kufanikisha upatikanaji wa umeme kwa Waafrika milioni 300 ifikapo mwaka 2030," alisema Msigwa huku akionesha juhudi za ushirikiano na washirika wa kimataifa kama Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), na Umoja wa Afrika (AU).

Alisema majadiliano ya mkutano huo yatagusia masuala muhimu ikiwamo maendeleo ya vyanzo vya nishati mbadala, upanuzi wa upatikanaji wa umeme vijijini na mijini na uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda afya ya umma na mazingira.

Alisema kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia, Tanzania inalenga kuhakikisha asilimia 80 ya kaya zinapata suluhisho la nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Msigwa alisisitiza mafanikio ya Tanzania kuongeza upatikanaji wa umeme vijijini, ambako zaidi ya asilimia 99 ya vijiji sasa vimefikiwa, huku zaidi ya vitongoji 32,000 vikiwa vimeunganishwa na gridi ya taifa na kwamba mafanikio hayo yameleta maboresho makubwa katika sekta za afya, elimu, na uchumi nchini na kutoa msingi wa ukuaji zaidi. Pia alisema mkutano huo utatoa jukwaa kwa viongozi wa Afrika kusaini makubaliano muhimu yatakayobadilisha mazingira ya nishati barani humo. Marais wa Afrika 14 wanatarajiwa kuhudhuria mkutano huo.

Msigwa aliwataka waandishi wa habari kueneza taarifa sahihi kuhusu mkutano huo, akisisitiza umuhimu wa kuhamasisha uelewa wa umma ili kufanikisha malengo ya mkutano.

"Hii ni fursa ya kipekee kwa Tanzania kuimarisha nafasi yake duniani na kuonesha maendeleo tunayofanya katika sekta ya nishati. Tushirikiane kujenga taswira chanya ya nchi yetu na kuendeleza suluhisho endelevu za nishati kwa ajili ya mustakabali wetu," alisema Msigwa.

Balozi Noel Kaganda, Mkurugenzi wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, alisema kufikia Desemba mwaka jana, uzalishaji wa umeme Tanzania Bara ulikuwa umefikia megawati 3,169.20.

Kaganda, alisema upatikanaji wa umeme uliongezeka kutoka asilimia 14 mwaka 2011 hadi asilimia 78.4 mwaka 2020 kutokana na juhudi za Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Mgombea CHADEMA apania kuwaunganisha wanawake

**Na Halfani Chusi**

MGOMBEA wa nafasi ya makamu Mwenyekiti Baraza la Wanawake Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (BAWACHA), Moza Ally amesema iwapo atashinda katika nafasi hiyo atahakikisha anashiriki kuwainua wanawake kiuchumi na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Moza alitoa kauli hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipoambatana na wenzake kurudisha fomu za kuwania nafasi mbalimbali katika ofisi ndogo za chama hicho zilizopo Wilaya ya Kinondoni.

Wengine waliorudisha fomu ni Michael Materu, anayewania nafasi ya Mweka Hazina Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), Masud Mambo, uenyekiti baraza hilo taifa na Revline Mbugi Unaibu Katibu Bara BAVICHA.

Moza, alisema amewania nafasi hiyo baada ya kubaini kuwa kuna pengo katika kuwahamasisha wanawake kuingia katika siasa.

"Uiamara wangu hauna shaka kama mnakumbuka nikiwa mkoani Mbeya nilisimama imara nikiwa BAVICHA, sasa nitakwenda kuimarisha BAWACHA kwa kushirikiana na kuhamasisha akina mama waliopo ndani na nje ya chama.

**"Uiamara wangu hauna shaka kama mnakumbuka nikiwa mkoani Mbeya nilisimama imara nikiwa BAVICHA, sasa nitakwenda kuimarisha BAWACHA kwa kushirikiana na kuhamasisha akina mama waliopo ndani na nje ya chama.**

"Ukiangalia nafasi mbili za juu za chama hakuna hata mwanamke mmoja aliyegombea, kwa hiyo tunajukumu la kuwajengea wanawake uwezo ili waweze kugombea nafasi za juu," alisema Moza ambaye kabla ya kutia nia katika nafasi hiyo alikuwa makamu mwenyekiti BAVICHA.

Alisisitiza kuwa iwapo atashinda katika nafasi hiyo, lengo lake katika chaguzi zijazo ni kugombea nafasi mbili za juu za uongozi ya Mwenyekiti Taifa na Makamu.

Mambo, alisema iwapo atashinda katika kinyang'anyiro cha uenyekiti BAVICHA Taifa, atasaidia kudai Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi nchini.

Vilevile, alisema atashiriki kupanga mikakati itakayosaidia BAVICHA ikiwamo kuinua vipaji kwa vijana na kuwahamasisha kuwania nafasi za kisiasa.

Katika ofisi za chama hicho, nderemo na vifijo vilitawala wakati wagombea hao wakirudisha fomu.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TPLB anzeni kwanza na upangaji wa matokeo kabla ya 'betting'

**KUMEKUWA** na wimbi kubwa la wanamichezo duniani kuingia katika michezo ya kubashiri na katika hilo, Shirikisho la Mpira wa Miguu duniani (FIFA), limekiri kwa sasa hilo ni tatizo kubwa, kwani limekuwa likififisha burudani, hivyo linalifanyia kazi ili kudhibiti kundi hilo.

Hata hivyo, FIFA imekiri kuwa inapata wakati mgumu kwani wakati mwingine wanamichezo hao hawabashiri wao moja kwa moja, bali wanashirikiana na raia wa kawaida na hata makampuni kwa ajili ya kuangalia maslahi yao.

Kwa mujibu wa kanuni za FIFA wanamichezo, kama vile wachezaji, waamuzi, makamisaa, viongozi wa klabu, makocha na mashirikisho, hawaruhusiwi kujihusisha katika michezo ya kubashiri kwani wakifanya hivyo wanaweza kuathiri matokeo ya michezo yenyewe uwanjani.

Tunajua wenzetu Ulaya wameendelea, wana vyombo na teknolojia ya hali ya juu kubaini wanamichezo ambao wanajishughulisha na kubashiri na tumesikia mara kwa mara wakiwabaini wachezaji, waamuzi na viongozi kabla ya kuwapa adhabu.

Pamoja na hayo bado FIFA wanakiri hadharani hali ni ngumu, kwani baadhi yao hawajihusishi moja kwa moja, wanapitia kwenye migongo ya watu wengine, hivyo ni ngumu sana kupata ushahidi.

Hivi karibuni tumemsikia Ofisa Mtendaji wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, akiulizwa maswali na baadhi ya waandishi wa habari kuhusu kuibuka kwa wanamichezo wa Tanzania nao kujihusisha na kubashiri.

Kasongo alisema wamesikia vitu kama hivyo, na akakiri kuwa jambo hilo linawasumbua hata huko Ulaya kwani halijawahi kuwa na ushahidi wa moja kwa moja, lakini tayari kuna kanuni ya kuwakataza wanamichezo kujihusisha na michezo hiyo ya kubashiri.

Alisema mpaka sasa hawajaliona, lakini kwa sababu wapo kwenye jamii, wanasikia vitu kama hivyo na kuahidi kulifuatilia kwa karibu.

Tunampongeza Kasongo kwa uthubutu wake, si wa kuonekana kupinga suala hilo, lakini pia kuahidi kuchukua hatua kama watapata ushahidi.

Hatupingi kwa TPLB na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kuanza kudili na wanamichezo wanaobashiri, lakini tunaona kunatakiwa ushirikiano mkubwa kwa wapenzi wote wa soka.

Tunadhani levo yetu kwa sasa ni kudili na upangaji wa matokeo kwanza ambao ndio unasikika na unaweza kupatikana ushahidi kama vyombo vyetu vitakuwa na dhamira ya dhati kwa hilo.


Kuwapo kwa kampuni moja inayodhamini klabu zipatazo sita kwenye Ligi Kuu huku moja kati ya hizo ikiweka mkono mkubwa zaidi, ni dalili mojawapo kuwa hatuko salama sana kwenye upangaji wa matokeo. Bado kuna timu zinaahidiwa kiasi cha pesa zinapocheza na baadhi ya timu tu, huku zikicheza na zingine huwezi kusikia hilo, hizi zote si dalili njema kwenye mpira wetu.

Na kwa bahati nzuri haya yote hayahitaji teknolojia ya hali ya juu kudhibiti, badala yake ni kusimamia misingi wa 'fair play' kuwa kampuni ambayo ina maslahi na timu moja isiruhusiwe kuzidhamini zingine, kuondoka ahadi za ujanjaujanja za pesa timu zikicheza na timu fulani, badala yake kama zinataka ziwekwe zinapocheza na timu zote kubwa, pamoja na kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa ajili ya kubaini waamuzi wanaopokea rushwa, wachezaji na hata viongozi wanaotoa kwa timu zingine.

Tunaamini hili linawezekana kama tukiwa na nia ya dhati kuliko la kubashiri. Bado kuna matatizo ya msingi sana kwenye soka letu ambayo hajapatia ufumbuzi kama haya. Tukiondoka huku tunadhani ndiyo twende kwa wanaobashiri. Wenzetu wameshaondokana na mambo ya kuuza au kununua mechi, ndiyo maana wameelekeza nguvu zao sasa huko.

Tuanze kwanza na tuhuma za kuuza na kununua mechi, pamoja na rushwa kwa waamuzi, haya ndiyo matatizo yetu ya msingi, mambo ya wanaobeti sawa yapigwe vita, TPLB ikiweka mkazo kwanza kwenye kilio cha udhamini huu ambao umekuwa ukipigiwa kelele kuwa na viashiria vya upangaji matokeo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kumbe inawezekana kupata Taifa Stars bora bila kupunguza wageni

**MECHI** ya ufunguzi wa Kombe la Mapinduzi kati ya Timu ya Tanzania Bara, Kilimanjaro Stars na Zanzibar Heroes, iliyochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Gombani, Zanzibar, imetuonesha kuwa inawezekana kabisa kuunda kikosi cha Taifa Stars bila kutengeza kanuni ya kupunguza wachezaji wa kigeni kwenye ligi yetu.

Ni mechi kali, iliyokuwa ya ufundi ambayo ilimalizika kwa Zanzibar Heroes kushinda bao 1-0, lililowekwa wavuni na, Feisal Salum maarufu kama 'Fei Toto.'

Achilia mbali matokeo ya mechi, wengi walioishuhudia walishangazwa na vipaji vya wachezaji wa Kitanzania kwa pande zote mbili, Bara na Visiwani.

Wachezaji wengi wametoka kwenye klabu za madaraja ya kati, na hakuna mchezaji yeyote aliyetoka Simba wala Yanga.

Waliocheza mechi ile waliwaonesha mashabiki kuwa mchezaji wa timu ya taifa, hapatikani kwa kurahisishiwa kazi kwa kuwabana wachezaji wa kigeni ili yeye aonekane.

Badala yake anatakiwa kuwekewa mazingira ya kushindana na hao hao wageni wenye uwezo ili aweze kupambana na kupata namba.

Kuna dhana imejengwa kuwa wachezaji wengi wa kigeni wanazuia wa Kitanzania kuonekana. Lakini ukiitazama sana dhana hii imejengwa sana kwenye Klabu za Simba na Yanga na kidogo Azam kwani ndizo timu zinazosajili wachezaji 12 wa kigeni.

Wanasema wageni wapunguzwe, pamoja na kwamba wanaongea kwa jumla, lakini lengo lao kubwa ni timu hizo tu. Kwa sababu kuna timu ya JKT Tanzania, Mashujaa, Prisons zote hizo hazina wachezaji wa kigeni, na zingine ambazo zinasajili wachezaji wa kigeni pungufu ya hao.

Pamoja na hayo, bado kuna kelele kutoka kwa baadhi ya mashabiki kuwa ni wengi sana. Wanachotaka ni kwamba Simba, Yanga na Azam ziwe na wachezaji wengi wa kizawa wawe wanapata namba kwa ajili ya kuitwa timu ya taifa.

Ni kama vile ni lazima mchezaji mzawa acheze au apitie Simba, Yanga ama Azam ili aitwe timu ya taifa.

Ukweli ni kwamba hakuna kanuni hiyo, badala yake kikosi cha Stars kinaundwa na wachezaji wa Kitanzania wanaocheza ligi ya ndani na nje ya nchi ambao wapo kwenye viwango bora kwa wakati huo wanaochaguliwa.

Hata kama hakutoka mchezaji wa Simba au Yanga kwenye kikosi cha Stars, bado haiondoi kuwa ni timu ya taifa. Ndiyo maana tunaona nchi za Afrika Magharibi kama Senegal, Nigeria, Ghana, wanaweza kuita kikosi kikawa na wachezaji wote wanaocheza soka la kulipwa barani Ulaya.

Nadhani na sisi taratibu tunaanza kuondoka huko japo bado watakuwapo wahafidhina ambao hivi majuzi walitaka kanuni ya kuwa na makipa wa ndani tu kwenye Ligi Kuu,

jambo ambalo lilipingwa na Rais wa Shirikisho wa Mpira wa Miguu nchini (TFF), Wallace Karia, akisema hawezi kuzipangia timu wawe na makipa wa aina gani, akisema kipa yeyote Mtanzania anatakiwa ashindane ili apate namba kwenye kikosi na si kuwekewa kanuni.

Kwa vikosi vya Kilimanjaro Stars na Zanzibar Heroes nilivyoviona, kunaweza kutengenezwa kikosi cha Taifa Stars bora kabisa ambacho kitafanya vema kwenye michuano ya CHAN, kama kitaongezwa na wachezaji wachache tu wazoefu kutoka Simba na Yanga.

Tanzania inaweza pia kuwa na kikosi bora zaidi kuelekea AFCON 2025 na 2027, kama wataongezwa pia wachezaji wanaocheza soka nje ya nchi ambao kwa sasa si haba.

Tuanze kuondokana na dhana kuwa wachezaji bora wenye uwezo wa kucheza Stars ni lazima watoke Simba au Yanga kwani tumeona hata timu za mikoani zinatoa wachezaji wazuri. Hata Zanzibar nako kuna wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu, tuziache Simba na Yanga na malengo yao, kwa kuwa si vitalu vya kutengeneza wachezaji wa Stars.

# LATRA yabaini magari ya kukodi yalipata ajali nyingi mwezi uliopita

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imefanya tathmini ya utoaji huduma za usafiri katika kipindi mwezi Desemba na kubaini kuwa magari mengi ya kukodi ndiyo yalipata ajali zaidi kuliko mabasi ya kawaida.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano LATRA, Salum Pazzy, kati ya ajali sita zilizotokea katika kipindi cha Desemba mwaka jana, tano zilihusisha mabasi madogo aina ya Coaster na mabasi ya kukodi huku moja ndiyo ilihusisha basi kubwa.

"Tathmini yetu imeonesha kuwa katika kipindi cha mwisho wa mwaka, hali ya utoaji huduma kwa abiria wanaokwenda kwenye mapumziko ya mwisho wa mwaka ilikwenda vizuri kwa sababu hakuna waliokosa usafiri na tunaamini TRC (Shirika la Reli Tanzania) kupitia treni za SGR na zile nyingine ilichangia kurahisisha utoaji huduma kuwa mzuri zaidi.

"Isipokuwa katika siku mbili za mwisho kabla ya Krismasi kulikuwa na msongamano mkubwa wa abiria na hivyo tulilazimika kutoa vibali vya muda kwa magari maalumu ya kukodi na abiria walipata usafiri.

"Lakini changamoto tuliyobaini ni ajali sita zilizogharimu maisha ya watanzania wenzetu, ambazo kati yake, ajali moja pekee ndiyo ilihusisha basi kubwa ambayo ilitokea maeneo ya Biharamulo, na ilihusisha basi likiwa limeegeshwa sehemu ambayo ilikuwa hatarishi, likarudi nyuma. Ajali tano kati ya hizo, zilihusisha mabasi madogo zikiwamo Coaster na mabasi ya 'special hire' (mabasi maalumu ya kukodi)."

Pazzy alisema katika tathmini hiyo walibaini kwamba sababu kubwa ya magari hayo ya kukodi kupata ajali ni kutofungwa Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Mabasi (TVS) pamoja na kifaa cha kufuatilia mwenendo wa dereva i-button. "Tumegundua kuwa kumekuwa na udanganyifu kwa aina hii ya mabasi ambayo yanatoa hizi huduma, tumebaini kwamba baadhi yao walikuwa wanabeba abiria wa kuokoteza mmoja mmoja kama yanavyobeba mabasi makubwa.

"Hivyo walikuwa wanakiuka masharti ya leseni zao, badala ya kusubiri kukodiwa au kutafuta kukodiwa, wao wamekuwa wakibeba abiria wa namna hiyo kwa kisingizio kwamba kulikuwa na uhitaji mkubwa wa huduma.

"Na pia wengine tumewakuta wakiwa na udanganyifu kwenye mfumo wa VTS au kwenye kutumia kitufe cha kufuatilia dereva (i-button), kwahiyo tumeendelea kufuatilia na kuchukua hatua kwa wote tunaowabaini ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini," alisema Pazzy.

Alisema kuwa kwa sasa wameanzisha kampeni maalumu ya kutoa elimu na kufunga mfumo wa VTS na i-button kwenye magari yote yanayobeba abiria.

"Kwahiyo katika maeneo yote haya ambayo tumegundua kuna udanganyifu, sasa tumeanzisha operesheni maalumu, tunaweka vituo maeneo ya njiani ambako magari hayo yanapita na maofisa wetu kwa kushirikiana na mafundi wa mfumo wa VTS na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani.

"Kwahiyo watakuwa wanasimamisha mabasi haya na kufanyiwa ukaguzi na wanapobaini kuna changamoto yoyote na wakiona kuna sababu ya msingi basi wanafanyia kazi," alisema.



Wakazi wa mtaa wa Majengo sokoni kata ya Uhuru jijini Dodoma wakiondoa taka zilizopo kwenye mfereji wa kupitishia maji jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Teknolojia saidizi, vifaa vyasambazwa kuboresha miundombinu wanafunzi wenye mahitaji maalumu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imenunua na kusambaza vifaa vya kielimu na teknolojia saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu ili kuhakikisha wanafunzi hao wanapata haki ya kujifunza katika mazingira wezeshi.

Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato, vishikwambi, digital voice recorder, bajiji, viti mwendo, fimbo nyeupe, obite reader na hansonatena saika.

Serikali pia imejenga na kukarabati miundombinu inayozingatia mahitaji maalumu ya wanafunzi kuanzia shule za awali mpaka vyuo vikuu uliokwenda sambamba na ujenzi wa shule jumuishi za mfano kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu -Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mafunzo ya kuwajengea uelewa wasaidizi wa wenye mahitaji maalumu kutoka taasisi za elimu ya juu zinazowapokea wanafunzi hao.

Alisema mpango huo wa serikali umelenga kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata fursa sawa za kujifunza na ustawi wao kwa ujumla ikiwa ni utekelezaji mkataba wa matamko ya kimataifa na kitaifa.

**Alisema mpango huo wa serikali umelenga kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanapata fursa sawa za kujifunza na ustawi wao ...**

Alisema katika kuhakikisha hilo linafanikiwa tayari serikali imefanya ujenzi wa shule jumuishi za mfano ikiwamo Shule ya Msingi Lukuledi iliyoko Halmashauri ya Masasi, mkoani Mtwara, Shule ya Sekondari Patandi (Arusha) na Shule ya Awali, Msingi na Sekondari Mbuye iliyoko Chato, mkoani Geita.

Alisema mpango mwingine wa serikali ni kuongeza vyuo vinavyotoa mafunzo ya elimu maalumu kwa walimu tarajali kutoka chuo pekee cha Patandi na kufikia vitatu, vikiwamo Mpwapwa na Kabanga na usambazaji vitabu vya kiada katika maandishi Braille yaliyokuzwa.


Mkurugenzi wa Elimu Maalumu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Magreth Matonya, alisema malengo ya mafunzo hayo ni kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu wanaingia shule mpaka vyuo vikuu na kumaliza kwa kiwango kinachotakiwa kwa kushirikiana na mawadeni (wasadizi wa wanafunzi).

Alisema katika kufikia lengo hilo, mawadeni kutoka katika vyuo 19 nchini, jumla yao wakiwa 147, wanapatiwa mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusiana na namna bora ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mkurugenzi huyo alisema mafunzo hayo yanatolewa kwa mawadeni ili wawalee wanafunzi kwa kiwango cha juu, hata kupata stadi na maarifa ya namna ya kukabilina na changamoto zinazowakuta wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mmoja wa mawadeni kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Cecilia Izahaki, alisema anahudumia wasioona, wenye ulemavu wa miguu na wasiosikia. Changamoto anayokumbana nayo ni kwamba wanafunzi hao hawapendi kuitwa majina kutokana na ulemavu wao.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



# Othman asifu ujenzi skuli ya ghorofa tatu kutoa fursa za elimu kwa Vijana

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema uimarishaji miundombinu kwenye maeneo mbalimbali ya Zanzibar ni kielelezo tosha kwamba skuli zinazojengwa zinalenga kutanua fursa ya elimu na kuhakikisha hakuna kijana wa Zanzibar anayekosa haki yake ya kupata elimu.

Othman ameyasema hayo huko Maungani Wilaya ya Magharibi "B" Unguja baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa skuli ya ghorofa tatu ya Maungani.

Alisema kwamba kufanya hivyo si tu kwamba ni kuwajenea misingi imara vijana wa Zanzibar katika kupata ujuzi na maarifa ya elimu, bali pia ni kujenga kizazi kitakachokuwa na uwezo wa kuchangia vyema maendeleo ya Zanzibar.

Othman aliongeza kuwa hali hiyo pia itawawezesha vijana kushindana vyema katika mabadiliko ya sasa ya ulimwenguni, hivyo ujenzi wa skuli hiyo na nyingine zinazojengwa ni sehemu ya jitihada za serikali katika kujibu changamoto ya elimu na kufanikisha azma ya kuleta maendeleo ya Zanzibar kwa vitendo.

Makamu wa Rais alisema Zanzibar imekuwa ni miongoni mwa nchi zenye ongezeko kubwa la watu, Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ikionesha ina wastani wa ongezeko la watu kwa asilimia 3.7 kwa mwaka.

Alisema hali hiyo inasababisha mahitaji na fursa ya elimu nayo kuongezeka maradufu mwaka hadi mwaka na hivyo kusababisha maeneo mengi ya Zanzibar kuwa na mahitaji makubwa zaidi ya madarasa ya kusomea kwa wanafunzi shuleni.

Alisema ujenzi wa skuli kama za Maungani na nyinginezo unatoa taswira kwamba serikali imeguswa na idadi ya watu na kwamba pia ongezeko la wanafunzi shuleni nalo ni kubwa na hivyo kufinya muda wa kujifunza, hivyo ujenzi huo ni suluhiso la changamoto hiyo ya uhaba wa madarasa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Leila Mohammed Mussa, alisema ujenzi huo ni jitihada za serikali katika kuleta mageuzi makubwa ya sekta ya elimu na kwamba kuwekeza katika elimu ni muhimu kwa kuwa hakuna taifa lolote linaloweza kuendelea pasi na watu wake kuwa na elimu.

Akitoa taarifa ya kitaalamu kuhusu ujenzi huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdalla Said alisema skuli hiyo itakuwa na uwezo wa kuchukua jumla wanafunzi 1,710 kwa wakati mmoja na kwa wastani wa darasa moja kwa watoto 45.




Katibu Mkuu wa Baraza la Wanawake Chadema, Catherine Ruge (katikati) akirudisha fomu ya kugombea nafasi hiyo kwa mara nyingine katika ofisi za CHADEMA Kanda ya Pwani, Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Kikwete akoshwa ushiriki wa wadau binafsi kwenye miradi ya maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS mstaafu Jakaya Kikwete amepongeza ushirikiano baina ya wadau binafsi na serikali katika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo, ikiwemo inayohusiana na afya, akibainisha kuwa hatua hiyo ni chachu muhimu zaidi katika kuchochea kasi ya maendeleo nchini.

Kikwete alitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki wakati akizindua rasmi Kituo cha Afya cha kisasa cha Kizimkazi, wilaya ya Kusini Unguja, kilichojengwa kwa ushirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na wadau mbalimbali, wakiwamo Taasisi ya Samia Foundation, Taasisi ya Ahmed Al Falas Foundation na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Hafla fupi ya uzinduzi wa kituo hicho chenye thamani ya Sh. bilioni 4.4 ilihudhuriwa na wadau mbalimbali wa sekta ya afya visiwani Zanzibar, wakiwamo Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, Katibu Mkuu Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Mngereza Mzee Miraji na viongozi mbalimbali waandamizi wa chama na serikali.

Walikuwapo viongozi na maofisa wa taasisi hizo wadau ambapo Taasisi ya Samia Foundation iliongozwa na mwenyekiti wa taasisi hiyo ambaye pia ndiyo mhandisi wa mradi huo, Fatma Kara, Mwakilishi wa Taasisi ya Ahmed Al Falas Foundation na maofisa wa Benki ya NBC wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Theobald Sabi pamoja na wananchi.

"Ushirikiano na ubia baina ya serikali na wadau mbalimbali ikiwemo taasisi binafsi ni njia rahisi zaidi katika kuchochea kasi ya maendeleo kwa faida ya wananchi.

"Ushirikiano wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi ya Samia Foundation, Taasisi ya Ahmed Al Falas Foundation na Benki ya NBC hadi kufanikisha mradi huu ni mwendelezo wa mifano mizuri ya kuigwa... hongereni sana!" Kikwete alipongeza.

Kikwete pia alipata wasaa wa kutembelea na kukagua sehemu mbalimbali za kituo hicho, akitoa wito kwa viongozi wa serikali na uongozi wa kituo hicho kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi sambamba na kutunza miundombinu mbalimbali ya kituo hicho ili kiendelee kutoa huduma bora inayosadifu dhamira ya kuanzishwa kwake.

"Kufuatia uzinduzi wa kituo hiki cha kisasa zaidi, matarajio ni kwamba wagonjwa wengi wa maeneo haya na jirani watapata huduma za afya hapa pasi na ulazima wa kwenda hospitali nyingine mbali kidogo na hapa.

"Hata hivyo, ipo haja ya kuhakikisha wataalamu wote muhimu wanapatikana hapa ili kuakisi nia njema za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi," alisisitiza Kikwete.

Awali, wakizungumza kwenye hafla hiyo, Waziri Mazrui na Katibu Mkuu Dk. Mngereza walisema uzinduzi huo ni sehemu ya maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwamba ujenzi wa kituo hicho utasaidia kuhudumia wananchi 13,000 kutoka maeneo ya Kizimkazi Mkunguni, Kibuteni, kizimkazi Dimbani na maeneo ya jirani.

Walisema ujenzi huo ndiyo utatumika kama kiwango sahihi cha ubora katika ujenzi wa vituo vingine vitakavyoendelea kujengwa visiwani Zanzibar.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Mbunge wa Viti Maalumu Mkoa wa Kusini Unguja na Mwenyekiti wa Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation, Wanu Hafidh Ameir alisema ujenzi wa kituo hicho cha afya kwa kiasi kikubwa utasaidia kusogeza huduma za afya kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo hususani wanawake ambao wengi wao walikuwa wanahofia kubeba ujauzito kutoka na huduma za afya kuwa mbali na makazi yao.

"Baada ya ujio wa kituo hiki ninaamini sasa wanawake wa eneo hili mtaongeza kasi ya kuzaa kwa kuwa idadi ya watoto waozaliwa eneo hili ipo chini sana kulinganishwa na maeneo mengine,'" alisema Wanu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi alisema ushiriki wa benki hiyo kwenye mradi huo ni mwendelezo wa jitihada zake kupitia sera yake ya Uwajibikaji kwa Jamii (Citizenship), ambapo benki hiyo imeeendelea kutenga sehemu ya faida yake kila mwaka ili kusaidia kutatua changamoto mbalimbali katika sekta za afya, elimu, mazingira, elimu ya fedha na ajira.

"Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, tumetoa zaidi ya Sh. bilioni nne kwa jamii. Leo, tunapozindua Kituo hiki cha Afya cha Kizimkazi, tunajivunia kuwa miongoni mwa wadau wakubwa waliofanikisha ujenzi wa kituo hiki muhimu.

"Tumechangia kiasi cha Sh. milioni 400 katika ujenzi wa kituo hiki ambacho kitaleta ahueni kubwa katika upatikanaji huduma bora za afya kwa wakazi wa Kizimkazi na maeneo jirani wakiwamo kinamama na watoto," alisema Sabi.

Naye Mhandisi Kara alisema nia ya Taasisi ya Samia Foundation ni kuhakikisha miradi kama hiyo inatekelezwa zaidi katika maeneo mbalimbali nchini.

## Wanafunzi kushindanishwa kumuenzi Shaaban Robert

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian ametangaza kumuenzi nguli wa fasihi ndani na nje ya nchi, Shaaban Robert kwa kuanzisha shindano kwa shule za msingi na sekondari mkoani hapa.

Balozi Batilda aliyasema hayo juzi wakati wa Tamasha la Kumbukizi ya kuzaliwa kwa gwiji huyo wa Kiswahili Duniani lililofanyika ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Alisema ameanzisha Shindano la Shaabani Robert ili kuenzi mchango wake.

Tamasha hilo lilijumuisha wazee wakiwemo wenye simulizi za maisha na falsafa za Shaaban Robert, watumishi wa umma, wajasiriamali na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Pongwe walioghani mashairi yenye maudhui yanayofanana nalo.

Mkuu huyo wa Mkoa, alisema washindi katika shindano hilo watapatiwa zawadi kama njia ya kuchochea ari ya kuandika na kusoma vitabu, riwaya, mashairi na kuziishi falsafa za Shaaban Robert. Awali Mtafiti wa Lugha Bakari Nauma alisoma wasifu wa marehemu Shaaban Robert uliogusia malezi katika familia, elimu na maeneo tofauti aliyofanya kazi ikiwemo Idara ya Forodha Pangani, alipokuwa na kipawa cha fasihi andishi, Idara ya Wanyamapori Mpwapwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Mwalimu Mussa Mayombe wa Shule ya Msingi Pongwe, alisema wapo wanafunzi wanaoshiriki nyanja mbalimbai zinazothibitisha kuwa na vipawa tofauti tofauti ikiwa ni pamoja na ushairi, hivyo ipo haja ya mpango kuwatambua na kuviendeleza vipawa vyao.

Omari Kombo, Mwalimu wa Kiswahili, alisema ni muhimu kuishi katika falsafa za Shaaban Robert kwa sababu zinaendelea kuishi.

# Manyara walia bei za sare za shule kupaa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BAADHI ya wakazi wa Mkoa wa Manyara wamedai kusikitishwa na kupanda gharama za vifaa vya shule za msingi na sekondari kwa mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti jana wakazi hao walidai kuwa wafanyabiashara wamepandisha bei maradufu ya sare za shule na viatu ikilinganishwa na mwaka jana.

Mkazi wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, Maulid Juma alidai baadhi ya wafanyabiashara wanatumia kipindi hiki cha mwanzo wa mwaka shule zinapofunguliwa kupata kipato zaidi.

Juma, alidai mwaka jana walikuwa wananunua jozi moja ya viatu kwa Sh.10,000, lakini kwa sasa imepanda hadi kufikia kati ya Sh.15,000 hadi Sh.20,000.

Mkazi mwingine, Enoti Philipo, alidai wafanyabishara hao wameingia tamaa kwa kupandisha bei ya bidhaa hizo na kusababisha sintofahamu miongoni kwao.

Alidai wafanyabishara hao wanapaswa kutambua kuwa kupandisha bei ya sare za shule na viatu siyo jambo zuri.

**"Mabegi ya shule unaambiwa kuanzia Shilingi 30,000 na kuendelea, bado sare za shule kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na madaftari juu," alilalamika Salmin.**

Mkazi wa Mjini Babati, Nurdin Salmin, alisema bei ya vifaa vya shule ni ghali tofauti na mwaka jana, kwani kwa mwaka huu gharama za vitu zimepanda mno.

"Mabegi ya shule unaambiwa kuanzia Shilingi 30,000 na kuendelea, bado sare za shule kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na madaftari juu," alilalamika Salmin.

Mfanyabiashara wa sare za shule katika mji mdogo wa Mirerani, Elias Jacob, alisema gharama haijapanda, kwani suruali za shule za sekondari wanauza Sh.20,000 na kaptura Sh.10,000.

"Bei ya mashati ya shule za sekondari ni Sh.10,000 na shule za msingi ni Sh.10,000 na viatu kuanzia Sh.15,000 na kuendelea," alisema Jacob.

Alisema kwa mwaka huu gharama ni ndogo ikilinganishwa na mwaka jana kwani bei hazijapanda, endapo kutakuwa na ongezeko ni kidogo mno.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka (kushoto) akizungumza kwenye tukio la kumpongeza Mwenyekiti wa kijiji cha Losoito, Samson Swakei lililofanyika kijijini hapo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Ulega ambana mkandarasi ujenzi kusuasua

**Na Oscar Assenga,** PANGANI

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega amemtaka Mkandarasi wa Kampuni ya M/s China Railway 15 Bureau Group Corporation kueleza sababu za kusuasua sehemu ya tatu ya ujenzi wa Barabara ya Ungamaa-Mkwaja -Mkange wilayani hapa Mkoa wa Tanga.

Ni baada ya kukagua sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 95.2 thamani ya Bilioni 111.55 na kubaini kuwa ujenzi wake unasuasua.

Njia hiyo ni sehemu ya barabara ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ipo kwenye ushoroba wa Pwani ya Afrika Mashariki kuanzia Malindi -Mombasa Lungalunga Kenya na Horohoro na Tanga-Pangani-Bagamoyo wenye urefu wa kilomita 454.

Hatua hiyo ya Waziri Ulega kumbana Mkandarasi huyo ilitokana na ziara yake ya kukagua maendeleo ya mradi wa Barabara ya Tanga-Pangani na Daraja la Pangani juzi akiwa ameambatana na viongozi waandamizi wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADs) na Mtendaji Mkuu, Mohamed Besta.

Akitoa maelezo kwa Waziri Ulega, mkandarasi huyo alitaja sababu kuwa ni mvua zinazonyesha na upatikanaji wa malighafi hasa kipande cha pili na cha tatu cha barabara.

"Ni kweli hatujafanya vizuri kwa sababu ya mvua nyingi kunyesha, hata upatikanaji wa malighafi hasa kipande cha pili na cha tatu cha barabara ni shida hali inayosababisha ujenzi kwenda kidogo kidogo," alisema

Waziri Ulega hakukubaliana na maelezo hayo na kusema ameangalia mtiririko wa mwenendo wa fedha kwenda kwa mkandarasi huyo na kubaini haidai fedha nyingi Serikali hadi kushindwa kutimiza majukumu yake hayo kwa wakati.

Akiwa katika ukaguzi wa Barabara ya Tanga-Pangani, alisema Serikali imetoa tena kiasi cha shilingi bilioni 4.7 ili mkandarasi wa Kampuni ya Chiko aendelee na kazi baada ya kusimama muda mrefu. Akizungumza wakati wa ziara hiyo Mbunge wa Tanga Mjini, Ummy Mwalimu alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kuendelea na kazi ya ujenzi

Ummy ambaye alikuwa eneo la Kirare jijini Tanga akimsubiri Waziri Ulega, aliwaeleza wananchi serikali imetoa fedha hizo ili ujenzi wa barabara hiyo uendelee.

"Mheshimiwa Waziri tufikishie salamu zetu kwa Rais, tunamshukuru sana kwa kutoa fedha hizi ambazo zitamfanya mkandarasi kurejea kazini na kazi ya ujenzi wa barabara hii utaendelea," alisema.

Alisema kukamilika kwa barabara hiyo ya Tanga- Pangani kutainua uchumi wa wilaya hizo.

Alisema wanaamini ujio wa Waziri Ulega utaharakisha ujenzi huo. Akizungumza katika eneo hilo, Ulega aliiomba kampuni ya Chiko kurudi na kurejesha mitambo yao ili waweze kuendelea na kazi ya ujenzi wa barabara hiyo ya kilomita 50.





# Kembaki: Katiba mpya sio kipaumbele cha Watanzania

**Na Samson Chacha,** TARIME

MBUNGE wa Tarime Mjini mkoani Mara, Michael Kembaki amesema Katiba mpya sio hitaji la wananchi bali wanataka amani na maendeleo.

Kembaki alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kujibu kauli iliyotolewa wakati wa sherehe za mwaka mpya mjini hapa na Mbunge wa Kurya Magharibi nchini Kenya, Mathias Rhobi.

Mbunge huyo alitoa kauli hiyo alipokuwa amealikwa kushiriki sherehe hizo nyumbani kwa Mjumbe Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Daniel Chonchori.

Alisema kwa sasa, Watanzania hawahitaji kupatiwa Katiba mpya na kuwa wakazi wa Jimbo la Tarime Mjini wanahitaji kujengewa barabara za lami.

Kauli hiyo imemuibua Kembaki na kuomba Mbunge huyo wa Kenya kuchukuliwa hatua kwa madai ya kutoa kauli za uchochezi mbele ya wananchi.

> **"Tumesikitishwa na kauli za mbunge Robhi aliyoitoa mbele ya umati uliohudhuria sherehe hiyo kuwa mji wetu hauna barabara za lami ...**

"Tumesikitishwa na kauli za mbunge Robhi aliyoitoa mbele ya umati uliohudhuria sherehe hiyo kuwa mji wetu hauna barabara za lami akimaanisha kuwa serikali haijafanya maendeleo," alisema Kembaki.

Alisema mji wa Tarime unajengwa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 18 na zinaongezwa kilomita nyingine sita na kufikia 24 na kuwa utakuwa na barabara za lami karibu asilimia 80 kufikia mwishoni mwa mwaka huu.

Alidai mahitaji mengine ya watu wa Tarime ni elimu, afya, barabara, utulivu, mshikamano na amani na kumtaka mbunge huyo kuacha kuwaletea siasa za nchini kwao.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Tarime, Novety Kibaji, alisema kauli za kuwataka Watanzania kupata Katiba mpya ni masuala yao wenyewe na Serikali sio ya watu kutoka nchi nyingine.

Chonchori, katika sherehe hiyo, aliwaalika marafiki zake muhimu, akiwemo Rhobi wa nchini Kenya na kusisitiza kuwa kauli alizotoa baada ya kupewa fursa ni zake binafsi.



Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Salum Hamduni (kushoto) akimkabidhi gari la kubeba wagonjwa juzi Mganga Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Dk. Nuru Yunge kwa niaba ya Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mkoa huo umepatiwa magari manne ya kubeba wagonjwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Wajumbe CCM waanza rafu ubunge, udiwani

**Na Ada Ouko,** BUTIAMA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilayani hapa Mkoa wa Mara, Marwa Siagi amewatahadharisha baadhi ya wajumbe wa chama hicho kuacha kuanza kufanya kampeni kugombea udiwani na ubunge kinyume na utaratibu.

Siagi alitoa tahadhari hiyo juzi kwenye kikao cha kawaida cha Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya hiyo.

Alisema kwa sasa katika wilaya hiyo hali ni mbaya kutokana na wajumbe hao na baadhi ya wanachama kukiuka kanuni na taratibu za chama kuwania nyadhifa hizo katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka huu.

"Wapo wanaoshangazwa na hali hii, kuna ambao wanashabikia huku wengine wakihoji wako wapi viongozi wa chama na nini kauli yao. Sasa niwaambie tu ni marufuku kufanya kampeni kabla ya muda," alisema.

Alisema watu hao wamekuwa wakitengeneza sababu zisizo rasmi kwa kuwaitwa wajumbe wa mkutano mkuu wa wilaya na kukutana nao kwenye madarasa.

Alisema wakiwa katika vikao vyao hivyo visivyo rasmi, wanatangaziana nia ya kugombea ubunge na udiwani na kumaliza kwa kulipana posho.

Siaga alisema baada ya hapo, wanakwenda kwenye miji na kuchinja ng'ombe.

Alisisitiza kuwa viongozi wa chama hicho wako macho na makini muda wote, kupitia kamati ya siasa ya wilaya hiyo, wamekutana na kutoa maelekezo ya kuzingatiwa baadae.

Alisema kuwa taratibu za chama hicho zinaeleza kuwa kwa wakati huu ambao rais, wabunge na madiwani wapo madarakani ni lazima watia nia wasubiri muda rasmi ukifika waanze shughuli zao.

Siaga, alisema uongozi wa chama hicho, umechukua hatua dhidi ya wajumbe na wanachama walioanza kunyemelea majimbo na kata kabla ya muda ili iwe fundisho kwa wengine.

Aliwataka viongozi na wajumbe wa halmashauri hiyo kudhibiti matukio hayo yasifanyike kwenye maeneo yao kwa kuwa muda wa kampeni haujafika.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa CCM Kata ya Bukabwa, Juma Nyamhanga, alisema wanaofanya hivyo watapoteza sifa kwa kuvuruga taratibu za chama hicho.

# Serikali yawanyooshea kidole madereva ambulance

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI mkoani hapa imeonya kuwa itawachukulia hatua kali madereva wa magari ya kubeba wagonjwa kwa kuendesha kwa mwendo kasi wakati hawajabeba wagonjwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Salum Hamduni alitoa onyo hilo juzi wakati akikabidhi magari manne ya wagonjwa, gari la chanjo na pikipiki 10 kwa waganga wakuu wa halmashauri za mkoa huo ili kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Hamduni, alisema madereva hao wamekuwa wakiendesha magari hayo kwa mwendo kasi wakati yakiwa hayana wagonjwa kinyume cha sheria na kanuni za usalama barabarani.

Alisema magari hayo ni kwa ajili ya dharura, hivyo madereva wasipokuwa na wagonjwa wala safari za kufuata wagonjwa wanatakiwa kuendesha taratibu na kwa kufuata sheria za barabarani.

Hamduni, alisema hali hiyo itawasaidia kuepukana na ajali za barabarani, kutohatarisha maisha ya watumiaji wengine wa barabara na vyombo husika kubaki imara kwa muda mrefu.

"Dereva ambayeataharibu magari haya kwa maksudi kwa kutozingatia sheria za usalama barabarani tutamchukulia hatua,"alisema.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Faustine Mlyutu, alisema vitendea kazi hivyo vimetolewa na Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuboresha utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Dk. Nuru Yunge, alisema gari la wagonjwa na pikipiki mbili, zitasaidia kuboresha huduma za afya kwa wananchi.

Nipashe
# Spotika



WAFUNGAJI 12 BORA LIGI KUU TANO ZA ULAYA 2024 UK. 12



ALEXANDER - ARNOLD

# WACHEZAJI WANAOTIKISA DIRISHA LA USAJILI JANUARI

**LONDON, England**

DIRISHA la usajili la Januari ni wakati mgumu sana kufanya biashara. Lakini ratiba iliyosheheni mechi, majeruhi, malipo au mvutano wa kusalia, hayo yote yanamaanisha makocha kadhaa wa Ligi Kuu England, huenda watahitaji kuingia sokoni msimu huu wa baridi.

Dirisha la uhamisho la Januari kwa klabu za Ligi Kuu England limefunguliwa Jumatano, Januari Mosi, na litafungwa Jumatatu ya Februari 3, mwaka huu.

Hapa tunawaangalia wachezaji watano wenye hadhi ya juu ambao mustakabali wao unaweza kuamuliwa mwezi huu.

**Trent Alexander - Arnold (Liverpool)**

Vyanzo vya habari vilisema katika mkesha wa mwaka mpya kwamba Real Madrid inataka kumsajili, Alexander-Arnold wa Liverpool Januari hii, lakini miamba hiyo ya Anfield imekataa.

Vyombo vya habari vya Hispania pia viliripoti kuwa Real walikuwa tayari kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa England mwezi huu.

Alexander-Arnold ni mmoja wa wachezaji watatu muhimu wa Liverpool ambao wapo kwenye miezi sita ya mwisho ya mkataba wao.

Arnold alisema Septemba kwamba mazungumzo juu ya mkataba mpya hayatafanyika hadharani, jambo ambalo limeongeza hali ya sintofahamu juu ya nini kinamkabili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa Liverpool tangu umri wa miaka sita.

Huku Liverpool wakipewa nafasi kubwa ya kushinda Ligi Kuu England, na wakionekana kufanya vizuri kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na wapo katika nusu fainali ya Kombe la Carabao, kuna uwezekano wa Real kukataliwa kumsajili kwa sasa - lakini hilo halitadumu kwa kwa muda mrefu.

Mkataba wake ni hadi Juni 2025 na anahusishwa na Real Madrid na Manchester City.

**Marcus Rashford (Man Utd)**

Kwa sasa swali ni lini Marcus Rashford ataondoka Manchester United? Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alisema katika mahojiano katikati ya Desemba kwamba "niko tayari kwa changamoto mpya" huku kukiwa na sintofahamu juu ya mustakabali wake Old Trafford.

Rashford amefunga mabao 138 katika mechi 426 alizoichezea klabu hiyo tangu aanze kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2016, ametokea katika timu ya vijana ya United. Msimu wa 2022-23 ndio wenye mafanikio zaidi alipofunga mabao 30 katika mechi zote.

Hata hivyo, ameshuka kiwango kwa muda wa miezi 18 iliyopita na kuvutia ukosoaji kutoka kwa wachambuzi na mashabiki. Rashford ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi United ambayo inaweza kuwa kikwazo kwa uhamisho wowote Januari hii.

Mkataba wake ni hadi Juni 2028 na anahusishwa na Paris St-Germain, Barcelona na klabu za Ligi Kuu ya Saudi Arabia, Al-Ahli, Al-Ittihad na Al-Qadsiah

**Martin Zubimendi (Real Sociedad)**

Kiungo wa Real Sociedad, Martin Zubimendi atakuwa mmoja wa wachezaji wa watakao vutia zaidi mwezi huu.

Liverpool walikuwa karibu kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 katika dirisha lililopita, lakini timu yake ilimtaka abaki.

Zubimendi, ambaye alikuwa kwenye kikosi cha Hispania kilichoshinda Euro 2024, inasemekana anauzwa kwa pauni milioni 51.7 katika mkataba wake. Akiwa na Sociedad hawezi kukosa ofa.

Mkataba wake ni hadi Juni 2027 na anahusishwa na Liverpool, Arsenal, Manchester City na Barcelona.

**Ben Chilwell (Chelsea)**

Ana umri wa miaka 28, Ben Chilwell, anapaswa kuwa katika kiwango cha juu kabisa cha maisha yake ya soka huko Chelsea, lakini badala yake amejikuta akipoteza nafasi yake katika kikosi cha kwanza pale Stamford Bridge chini ya kocha Enzo Maresca.

Chilwell, ambaye alijiunga na Chelsea kwa pauni milioni 45 kutoka Leicester mwaka 2020, amecheza kwa dakika 45 tu za mchezo wa Kombe la Carabao dhidi ya Barrow msimu huu, na hakuweza kuhama klabu hiyo katika dirisha lililopita.

Maresca alisema Chilwell ni miongoni mwa wachezaji "wanaofikiria kuondoka" na klabu "itajaribu kutafuta suluhu." Beki huyo wa kushoto, ambaye ameichezea England mechi 21, kwa mshahara wake kuna uwezekano mkubwa wa kuhamishwa kwa mkopo.

Amepewa mkataba hadi Juni 2027 na anahusishwa na Juventus, Brentford, Manchester United, West Ham na Fenerbahce

**Matheus Cunha (Wolves)**

Msimu wa 2024-25, umemfanya Matheus Cunha aonekane, ni msimu wa mapambano kwa Wolves.

Cunha amehusika katika mabao 11 katika mechi 11 zilizopita za Ligi Kuu England, akifunga mabao saba na kusaidia manne. Pia ndiye mchezaji wa kwanza wa Wolves kufunga mabao 16 ya ligi kuu ndani ya mwaka mmoja tangu John Richards afunge mabao 18 mwaka 1980.

Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 25, alisajiliwa kutoka Atletico Madrid kwa mkataba wa pauni milioni 35.

Amepewa mkataba hadi Juni 2027 na anahusishwa na: Liverpool, Arsenal, Manchester City, Manchester United na Newcastle

**Nani mwingine anaweza kuhama Januari?**

Kocha wa Chelsea, Maresca amesema Carney Chukwuemeka anauzwa na kiungo mwenzake Cesare Casadei anatolewa kwa mkopo.

Jaribio la Barca lililoshindikana kumsajili mlinzi wa Hispania, Dani Olmo, limetia shaka mustakabali wake katika klabu hiyo ya La Liga.

Mshambuliaji wa Newcastle, Alexander Isak amekuwa akihusishwa mara kwa mara na Arsenal. Florian Wirtz wa Bayer Leverkusen na Bruno Guimaraes wa Newcastle wote wamehusishwa na Manchester City.

Januari itakuwa dirisha la kwanza la uhamisho kwa kocha wa Manchester United, Ruben Amorim na anaweza kutaka kuleta wachezaji kadhaa ili kufanya mabadiliko.


Mshambuliaji wa Sporting, Viktor Gyokeres, amekuwa akihusishwa kuhamia Arsenal na United.

Mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee na winga Antony ni miongoni mwa wanaohusishwa kuondoka Old Trafford.

Mshambulizi wa Lille, Jonathan David mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu na ametajwa kuhusishwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England.

## ISIKUPITE

BAO alilofunga kinda Ethan Nwaneri dhidi ya Brighton juzi, limemfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga zaidi ya bao moja kwenye Ligi Kuu England akiwa na Arsenal kabla ya kutimiza miaka 18. Lakini pia linamfanya kuwa mchezaji wa sita kufunga bao zaidi ya moja katika historia ya ligi hiyo kabla ya kufikisha miaka 18 baada ya Wayne Rooney (mabao saba), Michael Owen (matano), Danny Cadamarteri (matatu), James Milner (matatu) na Federico Macheda (mawili).



# WAFUNGAJI 12 BORA LIGI KUU TANO ZA ULAYA 2024



HARRY KANE

**LONDON, England**

KUNA malalamiko mengi yanaweza kutolewa kuhusu soka la kisasa, kutoka kwa wingi hadi kupendekezwa kupungua kwa burudani, lakini hakuna ubishi kwamba mchezo huo bado umebarikiwa na kundi la wafungaji bora.

Hakika, kunaweza kuwa na upungufu wa namba tisa za kiwango cha juu, lakini mageuzi ya kimbinu yanamaanisha kuwa majukumu ya kufunga hayataangukia tu kwa mtu mmoja.

Kwa hiyo, kuna uwiano mzuri kati ya wachezaji wanaocheza namba tisa na washambuliaji wanaoweza kunyumbulika.

Makala haya inawaangalia wafungaji 12 bora kutoka ligi tano bora za Ulaya kwa mwaka 2024.

**Lois Openda (RB Leipzig), Michezo: 33, Mabao: 19**
**Dakika kwa kila bao: 142**

Mazungumzo mengi kuhusu RB Leipzig mnamo 2024 yalionekana kumlenga, Benjamin Sesko raia wa Slovenia mwenye umri wa miaka 21.

Lakini baada ya kucheza vizuri kwenye Ligue 1 akiwa na Lens, Openda amepiga hatua kubwa zaidi. Yeye hodari wa kuongoza mashambulizi. Mbelgiji huyo ana kasi ya kuwaka, lakini pia ni mwenye jicho zuri la bao.

Huku Sesko akifunga mabao 17 katika Bundesliga mnamo 2024, Openda alifunga mabao 19.

**Ante Budimir (Osasuna),**
**Michezo: 33, Mabao: 19**
**Dakika kwa kila bao: 131**

Budimir alitesa kwenye Ligi ya Daraja la Pili ya Ujerumani, Italia na Hispania, lakini mshambuliaji huyo wa Croatia amepata nyumba ya muda mrefu pale Osasuna.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, alifurahia msimu wa 2023/24 alipofunga mabao 17 kwenye LaLiga. Kiwango chake cha kushambulia kimeimarika tu msimu wa 2024/25 - mabao 10 katika michezo 18.

**Vinicius Junior (Real Madrid),**
**Michezo: 30, Mabao: 19**
**Dakika kwa kila bao: 118**

Namba za Mbrazil huyo labda si za kuvutia ikizingatiwa kwamba watu wengi walidhani alinyimwa tuzo ya Ballon d'Or ya 2024. Vini alifunga mara 19 katika mechi 30 za LaLiga mnamo 2024 na alifanikiwa katika kipindi cha kwanza cha mwaka huku Real Madrid ikitwaa taji lingine la ligi.

Winga huyo bila shaka alikuwa mchezaji bora zaidi duniani kwa muda mfupi baada ya kurejea kutoka kwenye jeraha la paja mwaka mpya, akifunga katika ushindi muhimu dhidi ya Girona na Barcelona.

Idadi ya mabao yake ilikamilishwa na pasi za mabao za mara kwa mara na uchezaji wa kutosha katika hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Licha ya ujio wa Mfaransa Kylian Mbappe, Vini Jr ameendelea kuthibitisha kuwa yeye bi bora zaidi pale Real Madrid.

**Kylian Mbappe (PSG/Real Madrid), Michezo: 29, Mabao: 19**
**Dakika kwa kila bao: 115**

Mbappe alitawala vichwa vya habari vya majira ya joto kwa kukamilisha uhamisho wake uliosubiriwa kwa muda mrefu katika mji mkuu wa Hispania, Madrid, lakini supastaa huyo wa Ufaransa bila shaka hakuanza vizuri Madrid.

Mabao 10 katika mechi 16 za LaLiga ni kurudi kwa heshima, lakini wengine walitarajia namba kama za Erling Haaland za msimu wa 2022/23 katika mwaka wa kwanza. Hata walio bora zaidi wanapaswa kuzoea, na Mbappe amelazimika kuzoea kufanya kazi ili aweze kujiamini.

Kiwango cha mshambuliaji huyo mwishoni mwa 2024 kinaonesha kuwa ana mengi mazuri kwa mwaka 2025.

**Mohamed Salah (Liverpool),**
**Michezo: 31, Mabao: 23**
**Dakika kwa kila bao: 107**

Mmisri huyo yupo kwenye kilele cha ubora kwenye Ligi Kuu England.

Msimu wa 2024/25 hadi sasa, Salah amerekodi michango 30 ya mabao (pamoja na mabao 17) katika michezo 18 ya viongozi hao wa ligi.

Liverpool bila shaka wataweza kunyakua taji lao la pili la Ligi Kuu ikiwa Salah ataweza kukaribia kufikia matokeo yake katika kipindi cha pili cha msimu, lakini winga huyo alipunguza kasi katika kipindi cha mwisho cha utawala wa Jurgen Klopp - hasa kutokana na kuumia kwa misuli ya paja.

**Alexander Isak (Newcastle),**
**Michezo: 33, Mabao: 25**
**Dakika kwa kila bao: 107**

Huyu ni mnyama kwelikweli na ameonesha thamani ya pauni milioni 150 ambayo Newcastle United wanaitaka kama atauzwa. Mustakabali wake unaweza kutegemea ikiwa klabu hiyo itafuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Raia huyo wa Sweden hakika anafanya kila awezalo kulirudisha jeshi la Newcastle kwenye nchi ya ahadi.

Wakati sehemu ya mabao 25 ya Isak ya Ligi Kuu ya England mwaka 2024 yalifika Desemba ambapo alifunga mfululizo.

**Jonathan David (Lille),**
**Michezo: 32, Mabao: 25**
**Dakika kwa kila bao: 103**

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Canada amekuwa na msimamo wa kupachika mabao kwa Lille, na 2024 ilikuwa miezi 12 bora kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

David alifuatilia kampeni yake ya Ligue 1 ya mabao 24 kuanzia 2022/23 akiwa na mabao 19 msimu uliopita, na ameanza 2024/25 akiwa na 11.

**Alexander Sorloth (Villarreal/ Atletico Madrid)**
**Michezo: 36, Mabao: 25**
**Dakika kwa kila bao: 85**

Hakuna mchezaji aliyejumuishwa kwenye orodha hii aliyefunga mara nyingi zaidi ya Sorloth aliyecheza mara moja Crystal Palace mwaka 2024. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, alifunga bao kila baada ya dakika 85 kwenye LaLiga, huku mafanikio yake mengi akiyapata Villarreal kipindi cha pili cha msimu wa 2023/24.

Sorloth alifunga hat-trick dhidi ya Granada na Real Madrid kabla ya kujiunga na Atletico Madrid majira ya joto.

Bado hajashawishika katika mji mkuu wa Hispania, lakini mshambuliaji huyo wa Norway bado anajua lengo lilipo na mwaka wake wa kalenda uliisha kwa kiwango cha juu sana alipofunga bao la dakika za mwisho na kuwaangusha viongozi wa ligi Barcelona pale Katalunya.

**Cole Palmer (Chelsea),**
**Michezo: 36, Mabao: 26**
**Dakika kwa bao: 120**

Palmer alikuwa na wakati mzuri katika nusu ya kwanza ya msimu wa 2023/24 kabla ya kudumisha uzuri kama huo katika mwaka mzima wa kalenda.

Mchezaji huyo alifunga mara 26 katika mechi 36 za Ligi Kuu England kwa timu ya Chelsea.

Palmer haachi kufanya mambo yafanyike kila mara anapoingia uwanjani, na hakika hakukatishwa tamaa mnamo 2024.

**Erling Haaland (Man City),**
**Michezo: 35, Mabao: 27**
**Dakika kwa kila bao: 110**

Uwezo wa ajabu wa kufunga mabao wa Haaland ni wa kiwango cha juu kwa raia huyo wa Norway wakati wa miaka yake miwili ya kwanza pale Manchester City.

Alionekana kujiweka kileleni baada ya kuanza msimu wa 2024/25 na mabao matatu katika mechi kumi za mwisho za ligi katika mwaka wa kalenda yanamaanisha kuwa hafanyi masihara langoni.

**Robert Lewandowski (Barca),**
**Michezo: 37, Mabao: 27**
**Dakika kwa kila bao: 109**

Wakati Lewandowski alipunguza kasi kuelekea mwisho wa mwaka na kwa kweli alionesha kutokuwa na ufanisi mbele ya lango, nyota huyo mkongwe alicheza kwa kiwango cha juu zaidi katika miezi michache ya kwanza ya msimu wa 2024/25.

Kulikuwa na dalili za kupungua kuelekea mwisho wa umiliki wa Xavi huko Barcelona, na ushawishi wa raia huyo wa Poland ulikuwa mkubwa. Hata hivyo, awali alitiwa moyo na ujio wa Hansi Flick na amefanya kazi kwa utukufu pamoja na Raphinha.

Alianza msimu akiwa na mabao 14 katika mechi nyingi, lakini ana matatu katika mechi saba zake za hivi karibuni.

***Harry Kane (Bayern Munich),***
***Michezo: 30, Mabao: 29***
***Dakika kwa kila bao: 89***

Kampeni ya kihistoria ya Bayer Leverkusen ilimaanisha kwamba Kane hakukuwa na chake mwaka 2024 baada ya kuhamia Bayern Munich, lakini mshambuliaji huyo aliendelea kufanya kile anachofanya bora zaidi.

Mwingereza huyo alifunga bao la dakika chache tu kila dakika 90 kwenye Bundesliga alipomaliza kampeni yake ya kwanza nchini Ujerumani kwa kutwaa Kiatu cha Dhahabu, na Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya na Trophy Gerd Muller.

Hata hivyo, Kane, ambaye ana mabao 14 ya ligi katika mechi 14 hadi sasa msimu huu, hatimaye anaelekea kumaliza ukame wake wa mataji kupitia taji la Bundesliga huku Bayern wakiwa kileleni.

## Nukuu


"Tumesikitishwa sana na uamuzi ambao umewawezesha kupata bao kwa sababu sijawahi kuona kitu kama hiki maishani mwangu, Aligusa mpira pia. [Inashangaza]. Hiyo ina maana kwamba hatujawahi kuiona hapo awali. Sijaona katika kipindi changu kazini. Niliwauliza vijana kama wamewahi, na hakuna mtu aliyewahi kuona hili hapo awali. hivyo hii ni mpya," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, baada ya uamuzi wa mwamuzi Anthony Taylor, wakuipa Brighton penalti kwa kile alichodai wakati wakiwania mpira kwa kichwa William Saliba aliishia kumpiga kichwa Joao Pedro badala ya kuucheza mpira.**



"Bila shaka kuna shinikizo kubwa. Kwangu mimi, ni fahari na pia kiwango, ni vigumu zaidi wakati hatufanyi vizuri. Nitajitahidi niwezavyo, ninatoa kila kitu kusaidia klabu na tutafanikiwa. Najua ni vigumu kuelewa hilo kwa wakati huu, lakini tutafanikiwa," **Kocha wa Manchester United, Ruben Amorim, kabla ya kuivaa Liverpool jana kwenye mechi ya Ligi Kuu England.**



"Huu si wakati wa kufikiria sana kuhusu ubingwa, tunahitaji kuzingatia sisi wenyewe," **Beki wa Arsenal, Riccardo Calafiori, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 na Brighton kwenye mechi ya Ligi Kuu England juzi.**



Nipashe Spotika

NIPASHE JUMATATU JANUARI 6, 2025

# TIMU 5 ZILIZOSHANGAZA MASHABIKI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu unaanza, mashabiki wengi wa soka nchini walizitabiria timu nne, Simba, Yanga, Azam na hata Singida Black Stars kufanya vema. Na kweli, hadi mzunguko wa kwanza unamalizika zimefuatana kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Simba inaongoza ikiwa na pointi 40, ikiiacha Yanga kwa pointi moja tu, inayoshika nafasi ya pili kwa pointi 39. Azam ni ya tatu ikiwa na pointi 36, huku Singida Black Stars ikikalia nafasi ya nne na pointi zake 33.

Baada ya hapo kuna timu ambazo zina mazoea ya kutikisa maeneo ya kati ya ligi kila msimu, mfano msimu uliopita Coastal Union ikifanya hivyo hadi kufanikiwa kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, KMC, Kagera Sugar na zingine.

Hata hivyo, msimu huu umekuwa tofauti. Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza kuna timu ambazo zimeonekana kuwa tishio kwenye Ligi Kuu na kushangaza mashabiki wengi kutokana na si tu kuwa sehemu nzuri kwenye msimamo wa ligi, bali hata upinzani zinaoutoa, tofauti na msimu uliopita ambapo baadhi yake ziliponea chupuchupu kushuka daraja, zingine zikiponea kwenye 'play off.' Hebu tuziangalie timu hizo, kazi zilizozifanya hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza...



Kikosi cha Tabora United kabla ya kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, Novemba 7, mwaka jana na kushinda mabao 3-1.

**1# Tabora United**

Imekuwa ni moja kati ya timu tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kushangaza wengi. Ndiyo timu iliyowafunga Mabingwa Watetezi, Yanga mabao 3-1, ikifanya hivyo Novemba 7, mwaka jana, Uwanja wa Azam Complex, Dar es salaam, kwenye mchezo wa ligi na kuwaacha wengi midomo wazi.

Si jambo la kawaida kwa timu kubwa za Simba na Yanga kufungwa idadi kubwa ya mabao kama hayo na timu za daraja la kati kama hiyo.

Ikaifunga pia, Azam mabao 2-1 katika mchezo uliochezwa, Desemba 13, mwaka jana, ikiwa nyumbani, na kuilazimisha sare ya mabao 2-2, Singida Black Stars, ambayo ilikuwa inaongoza mabao 2-0 hadi kipindi cha pili.

Ni timu ambayo haikutarajiwa kufanya maajabu hayo hadi mzunguko wa kwanza kwani msimu uliopita, ilimaliza ligi ikiwa nafasi ya 14 na kucheza mechi ya mchujo dhidi ya JKT Tanzania, ikachapwa mabao 4-0 nyumbani, kabla ya kulazimisha sare ugenini, kiasi cha kulazimika kwenda kucheza 'play off' ya pili dhidi ya Biashara United iliyotoka Ligi ya Championship.

Ililazimika kushinda mabao 2-0 nyumbani, baada ya kupoteza bao 1-0 ugenini, na kupata ushindi wa jumla wa mabao 2-1 ulioibakisha Ligi Kuu. Hadi inamaliza mzunguko wa kwanza msimu huu, ipo nafasi ya tano nyuma ya Singida Black Stars, ikiwa na ponti 25.

**2# Mashujaa FC**

Huu ni msimu wa pili inacheza Ligi Kuu Tanzania Bara. Msimu uliopita pamoja na kuanza vizuri michezo ya mwanzo, ilianza kufanya vibaya kwenye mechi nyingi zilizofuatia kiasi cha kudhaniwa kuwa inaweza kushuka daraja.

Ushindi wa michezo mitatu mfululizo ya mwisho, na ule wa mwisho dhidi ya Dodoma Jiji ilioshinda mabao 3-0 uliifanya kufikisha pointi 35 na kushika nafasi ya nane kwenye msimamo, ikikwepa kwenda 'play off', ikisaidiwa pia na matokeo ya michezo mingine ya kumaliza msimu ilioicha salama.

Haikudhaniwa kuwa mpaka mzunguko wa kwanza msimu huu inaweza kuwa 'ngangari', kwani ipo nafasi ya saba, ikiwa na pointi 19 kwa michezo 16 iliyocheza.

**3# JKT Tanzania**

Ni moja kati ya timu ambazo nusura ziteremke daraja mwaka jana. Mechi ya mwisho ya kumaliza msimu ilikutana na kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Simba, Mei 28, mwaka jana.

Kipigo hicho kiliifanya kumaliza nafasi ya 13 kwenye msimamo ikimaliza ligi na pointi 32, ikamalizika kwenda kucheza mechi ya mchujo na Tabora United iliyomaliza nafasi ya 14.

Kwa bahati nzuri ilishinda mabao 4-0 ikiwa ugenini, Ali Hassan Mwinyi, Tabora na kulazimika 'kushikilia bomba' kwenye mchezo wa marudiano kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, ilazimisa suluhu ambayo iliibakisha Ligi Kuu.

Mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, imekuwa moja kati timu sumbufu kwenye Ligi Kuu.

Msimu uliopita ilifungwa mabao 5-0 na Yanga mzunguko wa kwanza, lakini huu ilifungwa mabao 2-0, ikicheza ikiwa pungufu, huku kipa wake namba moja akiwa amepigwa kadi nyekundu, ikatoka suluhu dhidi ya Azam, mechi ya mzunguko wa kwanza, sare ya bao 1-1 dhidi ya Singida Black Stars na kufungwa kwa taabu, dakika za majeruhi dhidi ya Simba, Desemba 24 mwaka jana.

Iko nafasi ya nane ya msimamo ikiwa imecheza mechi 16 na kukusanya pointi zake 19 mpaka sasa.

**4# Fountain Gate**

Ilionekana na mashabiki wengi wa soka nchini kama imefanya usajili wa kuungaunga. Ikumbukwe kuwa hii ndiyo ilikuwa Singida Big Stars ambayo wachezaji wake wengi mahiri walipelekwa kwenye timu ya Ihefu FC ya Mbarali, Mbeya.

Baadaye Ihefu ikiwa na wachezaji wengi wa Singida Big Stars, ilihamia Singida na ikabadilishwa jina ikawa Singida Black Stars, huku iliyobaki nayo ikaamuwa kujibadilisha jina na kuwa Fountain Gate, na maskani yake yakatoka Singida na kwenda mkoani Manyara.

Kutokana na kuchukuliwa na wachezaji wengi tegemeo, Fountain Gate haikutegemea kufanya lolote mpaka mzunguko wa kwanza kwani ilibaki bila kusajili wachezaji wenye majina makubwa au wengi kutoka nje ya nchi.

Kwa namna ya kushangaza ilianza Ligi Kuu kwa kishindo ambapo kuna wakati ilikuwa ikiongoza ligi hiyo.

Ni moja kati ya timu nne zilizofunga ambao mengi kwenye Ligi Kuu, ikiwa imepachika 24. Mastraika wake , Selemani Mwalimu mwenye mabao sita, na Edgar William aliyepachika mabao matano, wakiwa kwenye orodha ya wanaowania kiatu cha dhahabu. Yenyewe ipo nafasi ya sita kwenye msimamo ikiwa na pointi 20.

**5# Dodoma Jiji**

Inakamata nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, ikikusanya jumla ya pointi 19.

baada ya kutofanya vema kwa misimu miwili mfululizo, hakuna aliyetarajia kuwa ingeweza kuwa hapo ilipo mpaka sasa.

Msimu uliopita ilimaliza ikiwa nafasi ya 12, ikiwa na pointi 33, pointi moja tu juu ya JKT Tanzania iliyokwenda kucheza 'play off' na Tabora United.

Pamoja na kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Mashujaa FC katika mchezo wa mwisho, ilipona kwenda kucheza 'play off' kwa kuokolewa na Simba, iliyoifunga JKT Tanzania mabao 2-0 katika mchezo wa mwisho na kuibakisha ikiwa na pointi 32 iliyoilazimu kwenda kwenye mchujo na kuiacha Dodoma Jiji ikipeta.

**JE, WAJUA?**



BAO pekee alilofunga Alexander Isak wakati Newcastle ikiizamisha Tottenham 1-0 juzi, ni la 13 kwake msimu huu na katika mabao hayo 12 yamepatikana kwenye mechi 12 zilizopita kwa juhudi zake binafsi, hivyo kumfanya kuwa mchezaji wa tatu Newcastle baada ya Alan Shearer na Joe Willock, kuziona nyavu mara saba mfululizo katika Ligi Kuu England. Lakini pia Erling Haaland na Mohamed Salah ndio wachezaji pekee katika ligi hiyo wenye mabao mengi zaidi ya Isak wakati Cole Palmer na Bryan Mbeumo nao wakiwa na idadi sawa naye, mabao 13.



# Madaktari watibu watoto moyo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MADAKTARI wa Hospitali ya Rufaa ya Benjamini Mkapa (BMH), leo wanaanza kuwafanyia uchunguzi watoto na kutoa matibabu kwa watakaobainika kuwa na magonjwa ya moyo.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto wa BMH, Dk. Julieth Kabengula aliwaambia waandishi wa habari mwishoni mwa wiki iliyopita kuwa madaktari hao wanaanza kufanya uchunguzi huo katika kambi maalumu hospitalini hapo hadi Januari 10, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Dk. Kabengula, BMH itaendesha kambi hiyo pia kwa ajili ya kuwachunguza na kuwatibu watu wazima wenye matatizo ya moyo na wale wenye dalili za tatizo hilo ili kuhakikisha afya zao zinaimarika.

Alisema wazazi wanapaswa kuhakikisha watoto wote wenye dalili za kupumua kwa shida, kikohozi cha mara kwa mara, kutoongezeka uzito, kuchoka haraka na kushindwa kuhimili mazoezi kuwapeleka ili wafanyiwe uchunguzi na kupatiwa matibabu katika kambi hiyo.

Vilevile, aliwataka wazazi kuwapeleka watoto ambao hushindwa kunyonya na kutoka jasho jingi wakati wa kunyonya kufanyiwa uchunguzi ili kubaini kama wana matatizo waweze kupatiwa matibabu.

"Nitoe wito kwa wazazi na walezi kutoka viunga vyote vya Mkoa wa Dodoma na mikoa ya jirani kuwaleta watoto kuja kufanyiwa uchunguzi na kupata matibabu ya magonjwa ya moyo," alisema Dk. Kabengula.

Aliwataka watu wazima wenye kisukari, shinikizo la juu la damu, matundu kwenye moyo, dalili za kukosa pumzi na mapigo ya moyo kwenda mbio kufika katika kambi hiyo kupata huduma.

Awali, alisema kambi zinazofanywa na madaktari bingwa wa magonjwa katika hospitali hiyo zinatokana na uwekezaji kwenye sekta ya afya uliofanywa na serikali ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya bora.

# Mbunge 'atema nyongo' upigaji fedha za Mfuko wa Jimbo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MBUNGE wa Singida Kaskazini, Ramadhani Ighondo ameonesha kushtushwa na matumizi mabaya ya Fedha za Mfuko wa Jimbo katika ujenzi wa baadhi ya miradi na kuagiza mamlaka husika kuchukua hatua kwa waliohusika na ufujaji.

Mbunge huyo alishtukia upigaji huo baada ya kutembelea miradi hiyo inayojengwa yenye thamani ya Sh. milioni 88.6 akiwa na Kamati ya Mfuko wa Jimbo. Ighondo, alisema pamoja na kwamba mwaka huu ni wa Uchaguzi Mkuu, hakubaliani jinsi fedha hizo zilivyotumika kutokana na baadhi ya miradi kujengwa chini ya kiwango.

Mbunge huyo, alikataa mradi wa ujenzi wa shule shikizi iliyopo Kijiji cha Itaja kutokana na kutolingana na kiasi cha Sh. milioni 2.6 zilizotolewa.

"Sikubaliani na huu mradi hapa unaona kabisa hii sio sahihi naomba kupata maelezo kwa maandishi," alisema.

Mradi mwingine aliokataa ni ukarabati wa Shule ya Msingi Munkhola iliyopo Kata ya Mgori ambao ulipewa Sh. 500,000 kwa ajili ya kupaua chumba kimoja, lakini fedha zimeisha kabla ya kukamilika.

> **"Niwakumbushe tu kuwa nahitaji maandishi manunuzi na matumizi ya fedha zilizotoka katika Mfuko wa Jimbo," alisema.**

Mbunge huyo aliomba kupata taarifa za maandishi katika miradi hiyo akisema fedha zilizotumika ni za serikali ili kubaini wapi kumekaa sawa na wapi kuna mapungufu.

"Niwakumbushe tu kuwa nahitaji maandishi manunuzi na matumizi ya fedha zilizotoka katika Mfuko wa Jimbo," alisema.

Hata hivyo, Ighondo aliwapongeza wasimamizi wa ujenzi wa mradi wa nyumba ya Mwalimu wa Shule ya Msingi Mangida kwa gharama ya Sh.milioni 11 kutoka katika mfuko huo. "Niwapongeze sana kwa kazi nzuri mliyoifanya hapa hata mkituambia nataka kumalizia itakuwa rahisi kupata tena," Ighondo

Aliwataka wananchi kushirikiana katika usimamizi wa miradi ili iweze kujengwa vizuri kulingana na thamani ya fedha. Katibu wa Kamati ya Mfuko huo ambaye pia ni Ofisa Mipango wa Wilaya ya Singida Vijijini, Elia Simanjilo, alisisitiza kila mmoja aliyepitiwa na kupata fedha za miradi atawajibika kutoa taarifa ya manunuzi na matumizi.




Mzazi ambaye jina lake halikupatikana akichagua mabegi ya shule pamoja na watoto wake kama alivyokutwa eneo la barabara ya sabasaba jijini Dodoma mwisho wa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jiji kuwaondoa wafanyabiashara mbele ya maduka

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma inatarajia kufanya operesheni ya kuondoa bidhaa zinazopangwa mbele ya maduka, maeneo yasiyoruhusiwa na barabara za waenda kwa miguu.

Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Usimamizi wa taka ngumu Halmashauri hiyo, Dickson Kimaro, alitangaza mpango huo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara katika Kata ya Uhuru baada ya kumalizika kufanya usafi wa mazingira.

Kimaro, alisema operesheni hiyo itakuwa endelevu ili kuhakikisha maeneo ya jiji hilo yanakuwa wazi, salama na safi wakati wote.

Alisema bidhaa hizo zinazopangwa mbele ya maduka na maeneo hayo yasiyo ruhusiwa, zimekuwa kero pia kwa watumiaji wa vyombo vya moto, kukithiri uchafu wa mazingira na kuhatarisha maisha ya watu.

Vilevile, aliwataka wamiliki wa maduka kuacha tabia ya kujifungia majumbani wakati wa kufanya usafi wa mazingira kwenye maeneo yao.

Kwa upande mwingine, Kimaro, aliwataka wakazi wa jiji hilo kuwa mabalozi kuhamasisha usafi wa mazingira kwenye maeneo wanayoishi ili kuepuka kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko.

# UVCCM yahamasisha vyuo vikuu kusoma kwa bidii

**Na Mwandishi Wetu,** SINGIDA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Mkoa wa Singida umewataka wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani hapa kusoma kwa bidii na kuwa viongozi wa chama hicho na taifa baada ya kuhitimu masomo.

Katibu wa UVCCM wa Mkoa huo, Sebastian Maganga alitoa rai hiyo hayo juzi wakati wa Mkutano Mkuu wa Umoja huo Tawi la Seneti la Chuo cha Uhasibu (TIA) Kampasi ya Singida.

Maganga, alisema pamoja na mambo mengine, mkutano huo umejadili usajili wanachama wapya katika tawi hilo.

"Kuna watu wanne wamewekeza kwenu ambao ni mzazi, ndugu, CCM na serikali ambayo imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya juu kupitia Rais Dk. Samia Suluhu Hassan," alisema.

Maganga, alisema CCM imewekeza kwa vijana ikiamini wapo watakaokuwa viongozi ndani ya chama na serikali na hilo linawezekana iwapo wataonesha bidii kusoma.

"Hakikisheni mnasoma kwa bidii, mkumbuke kuwa Rais Samia amewekeza fedha nyingi katika Sekta ya Elimu kwa kuwajengea miundombinu bora na mikopo kwa ajili yenu vijana, hivyo jitumeni katika masomo acheni uzembe," alisema.

Aliwapongeza vijana wa Singida kwa kukipigania chama hicho katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika nchini Novemba 27, mwaka jana na kufanikisha ushindi mkubwa wa CCM wa zaidi ya asilimia 99.5.

Aliwaomba wanachama wa tawi hilo waendelee kuwaunganisha vijana wa vyuo kwa kufanya mikutano ya wanachama katika matawi yote ya vyuo na usajili wa wanachama.





# Kigogo wa CHADEMA, wenzake watimkia CCM

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

KATIBU Mwenezi wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Jimbo la Njombe Mjini, Kambarage Kayombo na wenzake saba wamekihama chama hicho na kutimkia Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kayombo alikuwa mgombea nafasi ya uenyekiti wa mtaa wa Kambarage kwa tiketi cha CHADEMA katika uchaguzi uliofanyika Novemba mwaka jana na kushindwa.

Mwaka 2020, pia aligombea udiwani wa Kata ya Njombe Mjini kupitia CHADEMA na kubwagwa.

Kayombo alirudisha fomu katika hafla iliyofanyika Kambarage mjini Njombe na kupokelewa na Katibu wa Siasa Itikadi Uenezi na Mafunzo CCM Mkoa wa Njombe, Josaya Luoga.

Akizungumza baada ya kuwapokea wanachama hao wapya, Luoga aliwaagiza kuanza kazi ya kukiimarisha chama hicho tawala mara moja.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa kadi ya CCM, Kayombo, alisema kilichomvutia kujiunga na chama hicho ni kutokana na uwepo wa katiba imara na yenye misingi ya kuigwa na nidhamu iliyopo.

**"Taifa linashuhudia chama kile cha CHADEMA kitu kinachoitwa utovu wa nidhamu, kwa hiyo sisi wengine tukaona wanatuchanganya tumeamua kuondoka," alisema Kayombo.**

Alidai CHADEMA kimekosa nidhamu kwa kuweka hadharani mambo ya kuyajadili ndani kwani hakuna yeyote anayeweza kufanikiwa bila kuwa na nidhamu.

"Taifa linashuhudia chama kile cha CHADEMA kitu kinachoitwa utovu wa nidhamu, kwa hiyo sisi wengine tukaona wanatuchanganya tumeamua kuondoka," alisema Kayombo.

Kayombo alisema katika Mkoa wa Njombe CHADEMA wamekuwa na mpasuko mkubwa hususani viongozi kwani kila mmoja anajiona ni mkubwa na hakuna vikao vinavyoweza kuyamaliza matatizo ndani ya chama.

Diwani wa Kata ya Njombe Mjini, Alatanga Nyagawa, alisema CCM kwa sasa imebadilika na haisumbui wananchi jambo linalovutia upinzani kuendelea kujiunga na chama hicho.

Baadhi ya wana CCM, akiwemo Solanus Mhagama, alisema uamuzi wanachama hao kujiunga na chama chao unawapa nguvu ya kuendelea kulitumikia taifa na kuwaletea wananchi maendeleo kwa wananchi.



. Mwenyekiti wa Kitongoji cha Majengo wilayani Muheza mkoani Tanga, Seif Twenye (Kulia) akijadili akizungumza na Mkandarasi wa kampuni inayojenga karavati katika barabara ya mtaa wa Mdote, Shauri moja mpaka Masaki Razack Mushi jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wazee wahimiza jamii kutunza mazingira

**Na Elizabeth John,**
WANGINGOMBE

WAZEE wa Kata ya Kipengere wilayani hapa Mkoa wa Njombe, wameitaka jamii kushirikiana kutunza na kulinda mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Wito huo waliutoa mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wakitoa pongezi kwa Mamlaka ya Uhifadhi Wanyamapori (TAWA) kwa kulinda na kutunza mazingira ya Hifadhi ya Mpanga Kipengere.

Mmoja wa wazee hao akiwemo, Lupelo Nyagawa, alisema hifadhi hiyo inalindwa na kuvutia wageni kufanya utalii wa ndani wa maporomoko ya maji yakiwemo ya Mto Kimani.

"Tunamuunga mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambaye anahimiza hifadhi za mazingira na utalii, jamii inapaswa kuja kujionea maajabu haya na uzuri wa vivutio vyetu," alisema Nyagawa.

Devotha Msigwa, alisema ili vivutio hivyo viendelee kuwepo, maeneo hayo yanapaswa kulindwa na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kujenga utamaduni kufanya utalii wa ndani mara kwa mara na kupongeza jitihada za serikali kukuza sekta ya utalii nchini.

Frank Chaula, aliiomba serikali kuendelea kutoa kipaumbele kwenye maeneo ya utalii kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Muongoza wageni ndani ya hifadhi hiyo, Innocent Makombe alifafanua kuwa mpanga ni neno mzee maarufu kama mpanga bure.

Alisema katika makazi yake alikuwa na miti mbalimbali ya matunda na misonge ya vivuli.

# Kamera kufungwa mabasi ya wanafunzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ameziagiza shule za msingi za binafsi mkoani hapa kufunga kamera kwenye mabasi yanayobeba wanafunzi ili kudhibiti ukatili kwa watoto.

Mtaka alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa kikao cha kamati ya ulinzi na usalama, wadau na viongozi wa serikali kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe.

Alisema ametoa agizo hilo kufuatia kuwapo kwa vitendo vya kikatili ambavyo vinafanyika kwenye magari hayo yanayobeba wanafunzi na mzazi anakuja kubaini pindi mtoto ameharibika. "Ndio kesi mnazoambiwa mtoto wa kwanza anachukuliwa saa 11 alfajiri kwenda shule, yupo yeye, dereva na konda. Na mtoto wa mwisho anarejeshwa nyumbani saa 12 jioni yupo yeye, dereva na konda," alisema na kuongeza kuwa:

"Wapo watoto wamepata changamoto ya ukatili wa kijinsia kwenye magari ya shuleni kwao."

Mkuu huyo wa mkoa, alisema hatarajii kuona mmiliki analalamika kuhusu gharama za kufunga kamera hiyo ya kurekodi matukio yanayofanyika kwenye basi lake kuwa kubwa kwa kuwa itasaidia ulinzi kwa watoto.

"Na mtoto anapolalamika tutakwenda kuangalia kwenye kamera. Maelekezo yangu Ofisa Elimu (Nelasi Mulungu) andika barua kwa shule binafsi za Mkoa wa Njombe zile ambazo magari yanachukua watoto wadogo kwa ajili ya kwenda shule zifungwe kamera kwa ajili ya kumuhakikishia mzazi wa mtoto wako yuko salama," alisema Mtaka.

Alisema kutoka na uwepo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) itasaidia kuondoa dhana ya wazazi na walimu kulaumiana bila ya sababu.

Vilevile, Mtaka alitoa rai kwa viongozi wa dini kuiokoa jamii dhidi ya vitendo vya ukatili kutokana na kuendelea kukithiri katika maeneo yao.

"Tupaze sauti kwenye nyumba za ibada, jamii ya wana Njombe ibadilike, tumekengeuka ni lazima ujumbe wetu sisi kama viongozi wa dini katika mahubiri yote tuwakumbushe watu wa Njombe mauaji, ukatili wa kijinsia, havimpendezi Mungu, tupaze sauti na sauti isikike," alisema.



# JK: Zanzibar ya zamani si ya sasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jakaya Mrisho Kikwete amesema Zanzibar ya zamani si ya sasa kutokana na kupiga hatua katika maendeleo.

Kikwete aliyasema hayo wakati wa hafla ya uwekaji jiwe la msingi Jengo la Utawala na Taaluma Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM) Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyofanyika eneo la Buyu nje ya mji wa Zanzibar mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema kasi ya maendeleo Zanzibar kwa sasa ni kubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alisema maendeleo yanaendelea kufanyika kwa kasi kwa Zanzibar na kuifanya ya zamani kutolingana na ya sasa kwa kupiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

Awali, Kikwete ambaye pia ni Mkuu wa chuo hicho, alisema bila ya uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan kupitia Mradi wa HIT unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) shughuli hiyo isingefanyika.

Alisema Rais Samia anastahili kupongezwa maana haikuwa rahisi kushajihisha taasisi hiyo kwenye mradi huo na kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Kikwete, alisema isingekuwa rahisi kufanyika kwa ujenzi huo bila ya kuwa na hatimiliki ya ardhi ya eneo la chuo hicho ambalo ni moja ya masharti ya benki hiyo. Alimpongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kufanikisha jambo hilo na ujenzi wa barabara.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo, umerahisisha usafiri kwa wanafunzi na wafanyakazi na kusisitiza kuwa Mwinyi hana mbadala wake katika utekelezaji wa ahadi zake za maendeleo.

Akiweka jiwe hilo la msingi katika jengo hilo, Rais Mwinyi, alisema katika Miaka 61 ya Mapinduzi, Zanzibar imepata maendeleo kila sekta ikiwemo ya elimu. Alisema sera kuu katika serikali yake ni uchumi wa buluu na katika sekta hiyo kuna utalii ambao unachangia pato la taifa kwa asilimia 30.

Alitaja sekta nyingine kuwa ni uvuvi, ukulima wa mwani na mazao ya baharini na kwamba chuo hicho ni muhimu kwa nchi kupata wataalamu hao.

Mwinyi alitaja sekta nyingine kuwa ni ya bandari, mafuta na gesi, usafiri na uzalishaji baharini.

Alisema taasisi ya chuo hicho ni muhimu kwa kuwa itatoa wataalamu wa uchumi wa buluu katika sekta hizo. Alisema matarajio yake ni kuwa chuo hicho kitatumia tafiti mbalimbali za uchumi huo wa buluu na wataalamu wake kupeleka tafiti hizo na kusaidia nchi kupata maendeleo.

Waziri wa Wizara ya Uchumi wa Buluu, Shabani Othaman, alisema kwenye sera ya uchumi wa buluu kuna vipaumbele vitano, vikiwemo uvuvi na ukulima wa mwani ikijumuisha mazao ya baharini.

Othaman, alisema ili kutimiza malengo katika vipaumbele hivyo, kunahitajika rasilimali watu, tafiti na teknolojia na utaalam. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, alisema katika mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu, serikali imewekeza katika uchumi wa buluu na kwa Zanzibar lazima izae matunda.

Lela, alisema wizara yake imeandaa mitaala na kutoa wanafunzi wenye sifa kujiunga katika chuo hicho. Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, alisema bila ya mapinduzi, mageuzi ya elimu yasingeweza kufikiwa.

Mkenda, alimpongeza Rais Mwinyi kwa kuhakikisha hakuna mkwamo katika ujenzi huo na serikali kwa kuanzisha Chuo cha Teknolojia ya ICT na kampasi ya chuo hicho cha kimataifa visiwani Zanzibar.

"Tunachofanya leo ni kuimarisha elimu ya chuo kikuu na taasisi ya elimu ya juu, "alisema.

Alisema chuo hicho kimepata mgao wa fedha shilingi bilioni 34.6 na kuvitaka vyuo vikuu kutoa digirii ya nadharia kuendana na mageuzi ya elimu.

Akitoa taarifa ya mradi huo, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Cha Dar es Salam Taasisi ya Sayansi ya Bahari, Profesa Willium Anangisye, alisema ni uwekezaji kwa lengo la kuimarisha taaluma ndani na nje ya nchi kiuchumi, kijamii na kiteknolojia.

Alisema pia ni mkakati wa chuo kuzalisha maarifa, utafiti na kuimarisha mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia kwa wanafunzi na wafanyakazi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Waziri asifu ujenzi wa barabara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrki Ramadhan Soraga amesema miundombunu bora ya barabara itamnufaisha mwananchi kiuchumi kwa kufanya biashara na kujiingizia kipato.

Soroga aliyasema hayo wakati akifungua barabara ya Bubwini Mafufu hadi Kiongwe Mkoa wa Kaskazini Unguja .

Alisema miundombinu imara na bora imekuwa kimbilio kwa wananchi hasa wa maeneo jirani kwa kufanya biashara na kukuza vipato vyao.

Alisema visiwa vya Zanzibar vimekuwa maarufu duniani kwa utalii, hivyo kuwepo kwa barabara za kisasa na zenye ubora ni nafasi muhimu kwa sekta hiyo.

Waziri huyo, alisema Serikali ya Zanzibar imeamua kujenga miundombinu imara ya barabara ili kuinua uchumi wa wananchi na kuongeza idadi ya watalii kutembelea vivutio visiwani hapa.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi , Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema serikali imeamua kujenga barabara kuu na za ndani ili kuwarahisishia wananchi usafiri kwa upande wa Unguja na Pemba.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akikata utepe kuzindua Kituo kipya cha Afya Kizimkazi, katika Wilaya ya Kusini Unguja mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake ni Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, na kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahamoud na wa pili kushoto ni Mama Salma Kikwete. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## ... ataka majengo ya hospitali ya kisasa

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

RAIS Mstaafu wa awamu ya nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Jakaya Kikwete amesema wakati umefika kwa Wizara ya Afya Zanzibar kujenga majengo bora na kisasa ya hospitali na vituo vya afya kulingana na wakati wa sasa .

Kikwete alitoa kauli hiyo wakati akizindua Kituo cha Afya Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja kilichojengwa na Samia Foundation.

Alisema kwa vile dunia inakwenda na wakati uliopo kwa sasa kuna ulazima wa majengo ya vituo vya afya na hospitali kujengwa kwa ubora wa hali ya juu. Alisema kituo hicho ni mkombozi kwa watu wa Kizimkazi kwa kupata huduma jirani.

Kikwete, alisema kituo hicho kitapunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali ya wilaya.

Kikwete alisema kuwa lengo kuu ni kuimarisha mfumo wa rufaa nchini na kuhakikisha huduma za afya zenye ubora zinatolewa kwa wananchi na wageni ukizingatia Zanzibar ni kisiwa cha utalii.

Alisema katika kuhakikisha huduma zinatolewa bila ya kusuasua ni matumaini ya kila mmoja kuwa uongozi wa Wizara ya Afya umefanya tathmini ya kina juu ya mahitaji ya wafanyakazi wanaohitajika.

Aliwataka wananchi kufuata maelekezo na utaratibu uliowekwa kutumia miundombinu iliyowekwa ili kupunguza gharama za matengenezo.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wizara hiyo imejipanga kujenga vituo kama hivyo 52 kwa Unguja na Pemba vya kisasa ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Mungereza Mzee Miraji, alisema hadi kukamilika, kituo hicho kimegharimu shilingi bilioni 8.7.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Samia Foundation, Fatma Kara, alisema kituo hicho kitatoa huduma mbalimbali ikiwemo mama na mtoto, upasuaji na uchunguzi wa maradhi.

# Mwingine atoweka, gari lake lakutwa limetelekezwa Buza

**Na Maulid Mmbaga**

MWANAMUME aliyetambuliwa kwa jina la Dastan Mutajura, amedaiwa kutoweka katika mazingira ya kutatanisha ikiwa ni siku ya pili sasa bila kuonekana huku gari lake likikutwa limetelekezwa.

Akizungumzia tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema kuwa Januari 4 mwaka huu, saa nane mchana, alipokea taarifa kutoka kwa wananchi ya kuonekana kwa gari aina ya Marcedes Benz lenye namba za usajili T 109 DVY.

Alisema kuwa baada ya kupokea taarifa hizo, polisi walifika hadi eneo la tukio na kukuta gari hilo limetelekezwa eneo la Buza Sigara, na kwamba taratibu zilifanyika na gari hilo lilivutwa hadi Kituo cha Polisi Buza.

"Baada ya taarifa kusambaa mapema leo (jana) katika Kituo cha Polisi Chang'ombe zimepokewa taarifa kutoka kwa ndugu kuwa gari hilo lililotelekezwa lilikuwa linaendeshwa na ndugu yao Dastan Mutajura, ambaye tangu Januari 4 mwaka huu alipoondoka kwenda kwenye shughuli zake, hakurejea nyumbani," alisema.

Hata hivyo, Kamanda Muliro alisema hatua za haraka zimechukuliwa katika kuhakikisha ufuatiliaji zaidi juu ya kutoonekana kwa Dastan unaendelea ili kujua nini kilichomkuta.

Kutekwa na kutoweka kwa watu katika mazingira ya kutatanisha ni miongoni mwa matukio ya kihalifu yaliyoripotiwa nchini mwaka jana, hata kuwapo rai mahususi ya viongozi wa madhehebu ya dini, wakitaka serikali ikomeshe kadhia hiyo.




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi mkoa wa Iringa Daud Yassin (katikati ) akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mambo mbali mbali kama sehemu ya kuanza mwaka. Kulia kwake ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Salim Asas na kushoto ni Katibu wa CCM mkoa wa Iringa Said Goha. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Makundi maalumu yapatiwa mikopo mamilioni ya shilingi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 357.3 kwa vikundi 60 vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa ajili ya kuwainua kiuchumi kupitia miradi mbalimbali ya ujasiriamali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Sharifa Nabalang'anya alisema mwishoni mwa wiki kuwa mikopo hiyo imetolewa ikiwa ni utekelezaji maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya uboreshaji mfumo wa utoaji mikopo ya asilimia10 kwa makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu nchini.

Alisema zaidi ya wananchi 300 watanufaika katika awamu ya kwanza na halmashauri itaendelea kutoa fedha kwa vikundi kulingana na upatikanaji fedha za mapato ya ndani ambazo zinatengwa kila mwezi.

"Malengo yetu ni kuona uwezeshaji wananchi kiuchumi ndani ya wilaya yetu unafikiwa," alisema Nabalang'anya.

Mkuu wa Wilaya ya Gairo, Jabiri Makame alisema kuwa kwa mwaka huu wa 2025, wilaya hiyo imejikita kuhamasisha wananchi kulima viazi mviringo kwa kuwa ni moja ya mazao ya kimkakati kwenye ukanda huo.

Makame alisema hayo baada ya kukutana na kufanya mazungumzo na Mwakilishi wa Kampuni ya na Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu Bora za Viazi Mviringo nchini katika ofisi zake mkoani Iringa.

"Tuna mkakati mkubwa wa uzalishaji wa zao la viazi mviringo katika ukanda wa Tarafa ya Nongwe ambako kilimo cha zao la parachichi kimekuwa na mvuto kwa wakulima," alisema Makame.

Alisema wakati wakulima wengi wa tarafa hiyo wanasubiri uzalishaji kwa wingi wa parachichi, kwa sasa wameshauriwa wajikite katika uzalishaji viazi mviringo kwa kuwa ni zao ambalo ni la muda mfupi na kwa mwaka wanaweza kuzalisha mara tatu kupitia kilimo cha umwagiliaji.

"Katika kipindi cha mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo kupitia fedha za mapato ya ndani, pamoja na Mbunge wa Gairo kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo watanunua mbegu za viazi mviringo," alisema Makame.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema mbegu hizo zitasambazwa kwa vikundi vya wakulima (vyama vya ushirika) katika Tarafa ya Nongwe kwa lengo la kutoa hamasa na kufungua fursa ya sekta ndogo ya viazi mviringo.

Makame alisema viazi hivyo vina soko kubwa katika miji mikubwa ya Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam na mingine midogo. Hivi sasa wakazi wa miji hiyo wanategemea viazi mviringo kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ambako ni mbali kulinganisha na Gairo ambayo ipo karibu zaidi na miji hiyo.

# Mkumbo: TIC lindeni wawekezaji wa ndani

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo amesisitiza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuhakikisha kinawalinda wawekezaji, hususani wa ndani, ili wasikwame katika uwekezaji wao nchini.

Prof. Mkumbo pia amekitaka kituo hicho kuwawezesha wawekezaji wa ndani pale panapostahili ili wasikwame kwa lengo la kukuza sekta ya uwekezaji kwa manufaa ya taifa.

Alieleza hayo jana alipotembelea moja ya viwanda mkoani Manyara, akisisitiza TIC kuwatazama wawekezaji kwa jicho la kipekee na kuhakikisha hawakwami kwa namna yoyote ile katika kufanikisha shughuli zao za kiuwekezaji.

"Niwaelekeze TIC wawekezaji kama hawa, wapeni jicho la pekee na kipaumbele uwekezaji wao usikwame hata dakika moja. Kile ambacho wanachotaka kufanikisha, tuwawezeshe wafanikiwe na tuahidi sisi kama serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji nchini," aliagiza.

Prof. Mkumbo alisema kuwawezesha wawekezaji kwa namna yoyote ile kutasaidia kufanikisha uwekezaji wao na kuingizia taifa kipato huku akiahidi kwamba serikali itaendelea kuwasikiliza na kushirikiana nao pindi wanatakapokutana na changamoto yoyote.

Waziri huyo pia alimpongeza mwekezaji huyo wa ndani wa kiwanda hicho, akimwahidi kwamba serikali itashirikiana naye kwa ukaribu ili kuhakikisha uwekezaji uliofanyika unakuwa na tija zaidi kwake na kwa taifa.

Prof. Mkumbo alikuwa mkoani Manyara kwa ziara ya kikazi ambayo ililenga kukagua na kuzindua miradi mbalimbali ya maendeleo.

**"Niwaelekeze TIC wawekezaji kama hawa, wapeni jicho la pekee na kipaumbele uwekezaji wao usikwame hata dakika moja. Kile ambacho wanachotaka kufanikisha, tuwawezeshe wafanikiwe na tuahidi sisi kama serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji nchini," aliagiza.**

# Gachagua ahoji kugeuzwa mbuzi wa kafara Kenya

**NAIROBI, Kenya**

ALIYEKUWA Naibu wa Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua amewajia juu wapinzani wake wa kisiasa akihoji ni vipi amekuwa mbuzi wa matatizo ya Kenya, huku akionesha kusikitishwa kwake na usaliti wa kisiasa kutoka kwa washirika wake wakati wa kuondolewa kwake madarakani.

Akizungumza katika ibada ya mazishi ya Eric Mutugi, mtoto wa aliyekuwa seneta wa Embu, Lenny Kivuti, Gachagua aliwapinga wabunge waliopotoshwa kwa kuamini kuwa kuondolewa kwake kutatatua masuala ya nchi hiyo na kuleta maendeleo.

Alifafanua zaidi kuwa hana kinyongo na wabunge hao, na kwamba hawapaswi kuomba msamaha kutoka kwake bali kutoka kwa watu waliomkabidhi kura zao.

"Unajua Spika wa Embu umesema niwasamehe walioniondoa madarakani, sina tatizo nao, hawakunikosea, waliodhulumiwa ndio walionipigia kura na hao ndio watu.

"Kwa hiyo, ukitaka amani, omba msamaha kwa wananchi. Sio mimi; Sina tatizo. Mimi ni mtu tu niliyechaguliwa. Sasa, ukiniondoa baada ya kuchaguliwa, hufikirii umewadhulumu walionichagua?," Gachagua alisema.

Kutokana na mabadiliko ya kisiasa, Gachagua aliwahakikishia wenyeji wa Mlima Kenya kuwa anasikiliza maswala yao kuhusu eneo hilo na kwamba yuko tayari kuwaongoza kusonga mbele.

Alielezea wasiwasi wake juu ya mustakabali wa mkoa huo, akionya kwamba wanaweza kujikuta katika kile alichoelezea kama shimo la sasa.

"Nimewasikiliza wazee, viongozi wa makanisa, wafanyabiashara na wataalamu, naendelea kusikiliza yanayojiri mashinani. Tutatoa mwelekeo kwa watu wa mlimani jinsi tutakavyoishi Kenya hii. Vinginevyo tunaweza tujipate kwenye shimo ambalo wametuweka, sawa," Gachagua alisema.

Awali, Gachagua alikanusha madai ya Kiongozi wa Wengi Bungeni Kimani Ichung'wah yanayomhusisha na utekaji nyara wa hivi majuzi.

Pia Gachagua alimshutumu Rais William Ruto na washirika wake kwa kutofautiana katika mzozo wa utekaji nyara, akiwataka viongozi wa Kenya Kwanza kuheshimu ujasusi wa Wakenya, akimshutumu Ichung'wah kwa kutumia uongo aliouita wa kipuuzi kumharibia jina.

***KTN***




Polisi wa Israel wakimwondoa mwandamanaji wakati wa maandamano ya kutaka kuachiliwa kwa mateka waliotekwa huko Gaza, nje ya makao makuu ya Wizara ya Ulinzi Tel Aviv juzi. **PICHA: AFP.**

# Israel yaua watu 200 saa 72 Gaza

**GAZA, Palesetina**

ZAIDI ya watu 200 wameuawa katika muda wa siku tatu zilizopita kutokana na mashambulizi yanayotekelezwa na Jeshi la Israel huko Ukanda wa Gaza kwenye majengo ya makazi, makundi ya watu wanaokusanyika mitaani, sokoni na ndani ya makazi yao.

Kwa mujibu wa taarifa za mamlaka ya Gaza jana pekee, zaidi ya watu 60 waliuawa. Na kinyume na matamshi ya Israel wanaodai walengwa wao ni watendaji wa Hamas, na kwamba katika kadhia hiyo wanawake na watoto ndio waathirika zaidi.

Mapema jioni jana, vikosi vya Israel viligonga mkusanyiko wa watu mbele ya kituo cha uokoaji katika kambi ya wakimbizi ya Bureij, ambayo ilikuwa shule ya Shirika la Umoja wa Mataifa la msaada kwa wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA), ambao walikuwa wakinunua chakula cha jioni kwenye duka la falafel.

"Shambulizi hilo la ndege zisizo na rubani liliua watu wanne na kujeruhi wengine wengi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo. Aidha, ilielezwa kuwa katika idara ya dharura kwenye Hospitali ya Martyrs ya Al-Aqsa, ilizidiwa na idadi kubwa ya watu, na kwamba baadhi waliachwa chini huku wengine wakisubiri kulazwa katika chumba cha upasuaji.

"Tayari ni damu nyingi imemwagwa, majeruhi ni wengi, na hakuna dawa za maumivu zinazopatikana hospitalini, pia kutokana na mashambulizi yanayoendelea, watu wanakufa kimya kimya kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vya matibabu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Hata hivyo, Waziri wa Ulinzi wa Israel Israel Katz alithibitisha kuwa mazungumzo yasiyo ya moja kwa moja na Hamas yameanza tena nchini Qatar kwa ajili ya kuwarejesha mateka waliokuwa wameshikiliwa huko Gaza.

Mkuu wa Hezbollah, Naim Qassem alisema kundi la waasi la Lebanon liko tayari kujibu ukiukaji wa mara kwa mara wa Israel wa usitishaji mapigano uliokubaliwa mwezi uliopita, huku kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Mataifa nchini Lebanon (UNIFIL) kikiishutumu Israel kwa vitendo vinavyo hatarisha mapatano hayo.

Vita vya Israel dhidi ya Gaza hadi jana vimeua Wapalestina wasiopungua 45,658 na kujeruhi 108,583 tangu Oktoba 7, 2023. Takriban watu 1,139 waliuawa nchini Israel wakati wa mashambulizi yaliyoongozwa na Hamas siku hiyo na zaidi ya 200 walichukuliwa mateka.

***Aljazeera***

# Russia yaahidi kuzidisha mashambulizi Ukraine

**MOSCOW, Russia**

MAMLAKA ya nchini Russia imeapa kulipiza kisasi baada ya kudai kuangusha makombora manane ya ATACMS yaliyotengenezwa na Marekani yaliyorushwa na Ukraine Jumamosi asubuhi kwa lengo la kulenga vitongoji vya nchi hiyo.

Wizara ya Ulinzi ya Russia jana ilisema vikosi vya ulinzi wa anga vya nchi hiyo vilidungua makombora manane ya balestiki pamoja na magari 72 ya angani yasiyokuwa na rubani (UAVs), ikisisitiza kuwa hatua hiyo ya serikali ya Kyiv, ambayo inaungwa mkono na wasimamizi wa Magharibi, itakabiliwa na kisasi.

Taarifa ya Wizara ya Ulinzi ilisema kwamba ndege kadhaa zisizo na rubani ziliharibiwa katika eneo la Leningrad kaskazini magharibi na moja huko Kursk, ambako Ukraine ilianzisha shambulio la kushtukiza mwishoni mwa msimu wa joto uliopita.

Ilielezwa kuwa Rais anayemaliza muda wake wa Marekani, Joe Biden aliidhinisha matumizi ya Kyiv ya ATACMS mwezi Novemba akisema kwa kiasi fulani ilikuwa katika kukabiliana na Russia kupanua mzozo huo kwa kupeleka wanajeshi wa Korea Kaskazini.

Hata hivyo, Rais wa Russia, Vladimir Putin alitishia kujibu mashambulizi ya Ukraine kwa kutumia ATACMS kwa kombora jipya la taifa hilo lenye uwezo wa nyuklia (Oreshnik).

Pia vyombo vya habari vya ndani vilisema mashambulizi ya ndege zisizo na rubani za Ukraine yalilazimu vizuizi vya muda kuanzishwa katika uwanja wa ndege wa St. Petersburg.

Gavana wa Mkoa wa Leningrad, Aleksandr Drozdenko, alisema katika taarifa kwenye Telegram kwamba "usiku na asubuhi ya Januari 4 zilivunja rekodi kwa idadi ya UAV zilizoharibiwa, na nne zilipigwa risasi kwenye eneo lake".

Wakati huo huo, kwa mujibu wa Kamandi ya Jeshi la Anga la Ukraine, Russia ilizindua jumla ya ndege zisizo na rubani 81 huko Ukraine usiku wa kuamkia Ijumaa hadi Jumamosi, zikiwemo ndege za Shahed zilizotengenezwa na Iran.

Vile vile, ilielezwa kuwa takriban ndege 34 za UAV na aina zingine za ndege zisizo na rubani zilidunguliwa, licha ya kusababisha uharibifu katika maeneo ya Chernihiv na Sumy. Ukraine inaingia mwaka huu kwa mguu wa nyuma katika mzozo huo, ulioanza mnamo Februari 2022, huku Russia ikipata mafanikio katika mstari wa mbele wa mashariki.

Ukraine pia ina wasiwasi kwamba utawala wa Trump unaokuja unaweza kukata misaada muhimu ya kijeshi, licha ya Trump mwenyewe kuapa kumaliza mzozo huo.

**CNN**

HABARIMICHEZO

# Prisons yamnasa kocha mkuu wa Geita Gold FC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI wowote, Prisons inatarajia kumtangaza Amani Josiah kutoka Geita Gold, kuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, badala ya Mbwana Makata ambaye imeamua kuachana naye.

Hiyo inafuatia taarifa ya Prisons hivi karibuni kuachana na Makata, huku Geita Gold nayo ikitangaza jana kusitisha mkataba na kocha wake huyo.

Taarifa ya Geita Gold iliyotolewa jana na Katibu Mtendaji wa Klabu hiyo, Ramadhani Bukambu, ilieleza kuwa imeridhia ombi la kocha huyo kusitisha mkataba wa kuitumikia klabu hiyo ambayo inashiriki Ligi ya Championship.

"Uongozi wa Geita Gold unapenda kujulisha umma kuwa umeridhia ombi la kocha Amani kusitisha mkataba wa kuendelea kuitumikia klabu yetu kama Kocha Mkuu.

"Maridhiano haya yamezingatia sababu za msingi ili kulinda maslahi ya pande zote mbili, hivyo kwa kipindi hiki timu itakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Choke Abeid," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Taarifa zinaeleza kuwa kocha huyo anakwenda kukinoa kikosi cha Prisons ambacho hakijafanya vizuri kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Uongozi wa timu yetu Prisons, umefikia makubaliano ya pande mbili kusitisha mkataba wa kazi na aliyekuwa kocha wetu, Mbwana na msaidizi wake Renatus Shija.

**"Kwa sasa timu itaongozwa na kocha, Shaaban Mtupa akisaidiana na wasaidizi wengine," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Prisons hivi karibuni.**

**Makata alianza kuinoa Prisons mwanzoni mwa msimu akichukuliwa kutoka Pamba Jiji ambayo aliipandisha daraja akiwa kocha mkuu.**

Prisons inashika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 14 kwa michezo 16 ambayo imecheza mpaka sasa.

# MASHAIRI YAPAMBA USIKU WA YALDA KITUO CHA UTAMADUNI IRAN

**Na Mary Geofrey**

KITUO cha Utamaduni cha Iran Dar es Salaam, kimeadhimisha sherehe za mwisho wa mwaka maarufu kama 'Yalda Night' kwa Wairani wanaoishi nchini, kwa njia ya burudani na kuenzi tamaduni zao.

Sherehe hizo zilizofanyika mwisho mwa 2024 katika kituo chao na kuhudhuriwa na Wairani kutoka maeneo mbalimbali nchini, ziliambatana na mashairi ya kiuajemi ya kale na kutoka Divan ya Hafez ambayo ni sehemu muhimu ya sherehe za Usiku wa Yulda.

Mkurugenzi Mkuu wa Kituo cha Iran, Dk. Mohsen Mareef, akizungumza wakati wa shamrashamra za shughuli hizo, alisema sherehe hiyo ilikuwa ni kumbukumbu yenye nguvu ya utambulisho wa kitamaduni na furaha ya kushiriki tamaduni katika mazingira ya tamaduni mbalimbali.

Aliwataka Wairani wote kutumia sherehe hizo kujenga madaraja ya kuelewana, kusherehekea ubinadamu wao wa pamoja na kufanya kazi kwa bidii huku wakiishi kwa usawa katika dunia yenye mila na tamaduni tofauti.

"Mwaka mpya ni fursa ya kukumbatia kuishi kwa pamoja na kuelewana miongoni mwa watu na mataifa. Mada za usiku wa Yalda ni mwanga juu ya giza, matumaini juu ya kukata tamaa, na umoja juu ya mgawanyiko, zinaweza kutumika duniani kote na kutufundisha umuhimu wa kukuza mshikamano na mapenzi mema," alisema Dk. Mareef.

Alieleza zaidi kuwa, sherehe hizo za utamaduni zilianza kwa kusoma mashairi ya Kiajemi ya Kale, ikiwa ni pamoja na mashairi kutoka Divan ya Hafez, ambayo ni sehemu muhimu ya sherehe za Usiku wa Yalda.

Alisema washiriki pia walifurahia vipindi vya kuhadithia hadithi zilizosimulia umuhimu wa kihistoria na Kitamaduni wa Yalda.

"Karamu ya kitamaduni, imezungukwa na komamanga, maboga, na vitafunwa vya Kiajemi, imeleta hali ya joto na mshikamano. Haikuwa tu ni wakati wa kuheshimu urithi wa Kiirani bali pia ni fursa ya kukuza uhusiano wa kina ndani ya jamii,"alisisitiza.

**IPO NAMNA HII...**



Kocha wa Timu ya Watoto ya Antas Sports, Sam Sanyagwa, akitoa maelekezo kabla ya kuanza mazoezi katika viwanja vya Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mgunda atembeza panga Namungo FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Juma Mgunda, amezidi kupitisha ,panga' kwenye kikosi chake ili kupata nafasi ya kukiboresha zaidi kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, ambapo safari hii ameamua kumtema kiungo mzoefu, Rafael Daud Loti.

Taarifa ya kumtema mchezaji huyo imekuja siku mbili tu baada ya klabu hiyo kuamua kuachana na wachezaji wanne, akiwamo, kiungo mkongwe, Frank Domayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya klabu hiyo iliyotolewa jana, imeamua kuachana na nyota huyo wa zamani wa Yanga, pamoja na Amade Momade, raia wa Msumbuji.

„Tumeamua kuchana na wachezaji hao, tunawatakia kila la heri katika majukumu yao mengine," ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Loti, alijiunga na Namungo, Julai 27, mwaka jana, akitokea Singida Big Stars, ambapo kabla ya hapo aliichezea Yanga ambayo alijiunga nayo, Julai Mosi, 2017 hadi alipotimkia Singida mwaka 2020.

Kiungo huyo ni mmoja wa wachezaji walioipandisha daraja, Mbeya City, ambapo aliichezea 2014, kabla ya kunyakuliwa na Yanga.

Siku mbili zilizopita, Namungo ilitangaza rasmi kuachana na wachezaji, Domayo, Amza Moubarack, Ritch Nkoli na Djuma Shaaban.

Wiki moja iliyopita, Djuma, beki wa kulia wa zamani wa Yanga na AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisema kuwa ameomba mwenyewe kuachwa ili akauguze majeraha yake kutokana na kukaa muda mrefu bila kucheza ndani ya kikosi hicho, lakini klabu ilikuwa haijatoa taarifa rasmi.

Wachezaji walioachwa na Namungo wanapishana na waliosajiliwa kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

Wachezaji hao ni Derrick Mukombozi, Emmanuel Charles na Najim Mussa ambaye yupo kwa mkopo akitokea Singida Black Stars. Namungo haijafanya vizuri sana kwenye michezo yake ya mzunguko wa kwanza, ikiwa tayari imeshacheza mechi 16, ikiwa nafasi ya 12 kwa pointi 17 ilizokusanya.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL YAKATAA OFA
KLABU ya Liverpool imekataa ofa ya pauni milioni 15 kutoka kwa Crystal Palace kwa ajili ya kumnunua Ben Doak. Kiungo huyo wa kati wa Scotland mwenye umri wa miaka 19 yuko kwa mkopo Middlesbrough. ***(Tme)***

### CUNHA ATAKIWA ARSENAL
KLABU ya Arsenal inachunguza uhamisho wa Januari kumnunua mshambuliaji wa Wolves na Brazil, Matheus Cunha, 25. ***(Football Insider)***

### PALACE KWA DIOUF
OFA ya Crystal Palace ya pauni milioni 12.4 ya kumnunua beki wa Senegal mwenye umri wa miaka 20, El Hadji Malick Diouf ilikataliwa. ***(Mercato Foot)***

### NEWCASTLE KUPATA FAIDA
KLABU ya Newcastle United inatazamiwa kupata faida kwa mara ya kwanza baada ya miaka mitano, lakini bado inapaswa kuuza wachezaji kabla ya kununua mwezi huu ikiwa watafuata sheria za kifedha za Ligi Kuu England. (***Subscription***)

### CHUKWUEMEKA NA NAPOLI
KLABU ya Napoli imeonesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Chelsea mwenye umri wa miaka 18, Carney Chukwuemeka, ambaye thamani yake ni takribani euro milioni 30. ***(TeamTalk)***

### KHUSANOV AWANIWA CITY
MANCHESTER City imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua beki wa Lens raia wa Uzbekistan, Abdukodir Khusanov, 20**.** ***(Telegraph)***

### LEMINA AWINDWA SAUDIA
KLABU ya Saudi Arabia, Al - Shabab ina uhakika wa kufikia makubaliano ya kumnunua kiungo wa kati wa Wolves mwenye umri wa miaka 31 raia wa Gabon, Mario Lemina. ***(Rudy Galetti)***

### POTER MKATABA MPYA
WINGA wa Brentford, Keane Lewis-Potter mwenye umri wa miaka 23, anakaribia kukubaliana na mkataba mpya. ***(Mail)***

### AGBADOU UHAKIKA
KLABU ya Wolves inatumaini kukamilisha usajili wa pauni milioni 15 wa beki wa kati wa Reims mwenye umri wa miaka 27, raia wa Ivory Coast, Emmanuel Agbadou mapema wiki ijayo. ***(Telegraph)***

### ONUACHU AWINDWA
KLABU ya Trabzonspor ya Uturuki inamtaka mshambuliaji wa Southampton, Paul Onuachu, 30. ***(Gunebakis)***

### SHEAF ATAJWA LEEDS
LEEDS United iko tayari kuwasilisha ofa kwa kiungo wa kati wa Coventry City, Ben Sheaf mwenye umri wa miaka 26, katika dirisha hili la Januari. ***(Leeds United News)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: KAMWE SIJAWAHI KUONA PENALTI KAMA HII

●●●Tumesikitishwa sana na uamuzi ambao umeleta bao, sijawahi kuona kitu kama hiki maishani...

**LONDON, England**

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema „sijawahi kuona" uamuzi wa ajabu kama penalti iliyotolewa kwa Brighton katika sare ya bao 1-1 ya timu yake kwenye Uwanja wa Amex Jumamosi.

Mshambuliaji wa Brighton, Joao Pedro, aligongana kichwa na William Saliba kwenye eneo la hatari na mwamuzi Anthony Taylor akamua kutoa penalti baada ya VAR kuthibitisha.

Na Pedro akafunga mkwaju wa penalti na kusawazisha matokeo kuwa 1-1, ambayo yalidumu hadi kipenga cha mwisho na kuwaacha Arsenal kwa pointi tano nyuma ya viongozi Liverpool ambao wamecheza michezo miwili pungufu kabla ya mechi yao ya jana dhidi ya Manchester United.

"Tumesikitishwa sana na uamuzi ambao umeleta bao kwa sababu sijawahi kuona kitu kama hiki maishani mwangu," alisema Arteta akiiambia BBC Sport baada ya mchezo huo.

Kocha huyo wa Hispania aliongeza kuwa wito huo wa penalti haukuwa wa kulaumiwa pekee kwa Arsenal kupoteza pointi kwa mara ya tisa kwenye ligi msimu huu, wakiwa hawajashinda mara 10 patika kipindi chote cha msimu wa 2023-24.

"Tulifanya mambo mengi si kwa kiwango na mpira, kwa hiyo hatukupata kasi yoyote, hatukujiweka katika maeneo ambayo baadaye tunaweza kutengeneza nafasi," alisema Arteta.

"Tuliruhusu nafasi moja tulipokuwa na wachezaji 10 na Yankuba Minteh akaondoka. Nadhani tunapaswa kufanya mambo mazuri zaidi kuliko leo (juzi) na kwa bahati mbaya tulipoteza pointi mbili."

Arsenal walikuwa wamepata bao la kuongoza katika kipindi cha kwanza kupitia kwa Ethan Nwaneri mwenye umri wa miaka 17, ambaye amekuwa mchezaji wa kwanza kuifungia klabu hiyo mabao mawili ya ligi kabla ya kufikisha miaka 18.

Nafasi ya Nwaneri ilichukuliwa na Gabriel Martinelli wakati wa mapumziko, na Arteta alithibitisha kwamba nyota huyo mchanga aliondolewa kwa wasiwasi wa „suala la misuli" katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

Arsenal na Arteta hawana muda mrefu wa kufanya tathmini baada ya sare ya Jumamosi kwani wako kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle United Jumanne.

HABARI MICHEZO



# Kocha Spurs: Nina hasira ya kufungwa

**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, alikasirika baada ya timu yake kufungwa tena kwenye Ligi Kuu England Jumamosi, lakini akisifia uchezaji wa timu yake iliyojaa majeruhi.

Kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Newcastle United haikuwa rahisi kwa Postecoglou akianza mwaka 2025 vibaya.

Huku mechi ya mkondo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Ligi ikikaribia dhidi ya Liverpool Jumatano na mechi inayofuata ya Ligi Kuu ugenini dhidi ya Arsenal, mambo yanaweza kuwa mabaya zaidi kwa raia huyo wa Australia.

Tottenham sasa wamepata pointi tano pekee katika mechi nane zilizopita za Ligi Kuu na kufikisha michezo sita ya ligi nyumbani bila ushindi.

"Ninajivunia sana uchezaji na nimevurugika hatukupata matokeo ambayo wachezaji walistahili, ilikuwa nzuri, bora na tulistahili kushinda," alisema Postecoglou, ambaye timu yake ina alama 24 kutoka kwa michezo 20, akiwaambia waandishi wa habari.

"Siku nyingine yoyote, kwenye uwanja wa haki na hata wa kuchezea, tungeshinda mchezo huu."

Postecoglou aliongeza: "Nimekasirika sana, na hasira zaidi nadhani nimewahi kuwa katika maisha yangu ya soka kiasi kwamba walinyimwa zawadi zinazofaa kwa uchezaji mzuri.

"Usiendelee kuniuliza kuhusu uamuzi. Kama nyie hamna maoni juu ya hilo ni sawa. Najua mnataka niseme tu.

"Ninachosema ni kwamba, siku yoyote kwa uwanja wa haki na hata wa kucheza na michakato ya mawazo yenye mantiki tungeshinda mchezo huo, ndivyo hivyo. Unaweza kufanya kile unachotaka kutoka kwa hilo."

# Evra ataka Maguire arudishiwe unahodha

**LAS VEGAS, Marekani**

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Patrice Evra, ameishauri klabu hiyo kumpa Harry Maguire kitambaa cha unahodha badala ya Bruno Fernandes.

Maisha ya beki huyo yalirejea kwenye mstari baada ya kipindi kigumu alipopoteza unahodha na nafasi yake kwenye kikosi cha Man United.

Maguire alipoteza nafasi yake kwenye timu ya Manchester United msimu wa 2022/23 chini ya Erik ten Hag. Wengine aliowapendekeza ni Lisandro Martinez na Raphael Varane.

Katika msimu wa majira ya joto wa 2023, wababe hao wa Kiingereza walikubali ombi kutoka kwa West Ham, lakini mwishowe aliamua kubaki kwenye timu hiyo.

"Nilikuwa tayari kubaki na kupigania nafasi yangu na tuna mabeki wa kati wanne au watano wakuu wa kimataifa na katika klabu hii na ushindani wa nafasi ni mkubwa sana," alinukuliwa kupitia The Independent.

Licha ya yote hayo, Maguire anachukuliwa kuwa mchezaji muhimu chini ya Ruben Amorim. Kocha huyo wa Ureno alisema wataongeza kandarasi yake kwa mwaka mmoja.

"Mrudishie kitambaa! 'Baada ya yote ambayo amepitia kuonesha ujasiri na uongozi," Evra alitoa maoni kwenye chapisho lake la Instagram.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ameanza mechi nne za mwisho za United na atakuwa mmoja wa majina ya kwanza kwenye mechi dhidi ya Liverpool. Alivaa kitambaa dhidi ya Newcastle na Everton.

# OLMO ATABAKI BARCELONA - FLICK

**BAERCELONA, Hispania**

KOCHA wa Barcelona, Hansi Flick, amesema bado ana imani kuwa Dani Olmo na Pau Victor wataweza kuichezea klabu hiyo tena msimu huu.

LaLiga na Shirikisho la Soka la Hiaspania walitangaza Jumamosi kuwa wamekataa ombi la Barca la kuwasajili tena wawili hao baada ya klabu hiyo ya Katalunya kutokizi vigezo vya sheria za ligi ya usawa wa fedha (FFP).

Olmo, aliyesajiliwa kwa euro milioni 60 majira ya kiangazi kutoka RB Leipzig, ana kipengele katika mkataba wake ambacho kitamruhusu kuondoka bila malipo ikiwa bado hajasajiliwa kwa kipindi cha pili cha msimu, lakini Flick amesema mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania amejitolea kwa Barca.

"Nina imani kuwa klabu itafanya hivyo," alisema Flick katika mkutano na waandishi wa habari baada ya ushindi wa mabao 4-0 wa Copa del Rey Jumamosi dhidi ya Barbastro, mechi ambayo Olmo na Victor wote walilazimika kukosa.

"Leo (juzi), nilizungumza na Dani na anataka kuchezea Barca. Tunamhitaji yeye na pia Pau Victor. Ni wachezaji wazuri sana. Tunawahitaji wote wawili. Inabidi tusubiri. Hili ndilo jambo pekee tunaloweza kufanya sasa. "

Mabao mawili kutoka kwa Robert Lewandowski na Eric Garcia na Pablo Torre yaliisaidia Barca kujikatia tiketi ya kuingia hatua ya 16 ya Copa.

"Nadhani kila mtu anataka wote wawili warudi kwa sababu ni wachezaji muhimu kwetu," aliongeza.

"Leo (juzi) tulicheza kwa umakini sana. Tulicheza kama tunavyotaka. Hakukuwa na kitu cha kuona au kuhisi kwamba timu iliteseka kuhusu hilo."

Beki Ronald Araujo, ambaye alicheza mechi yake ya kwanza msimu huu dhidi ya Barbastro, pia alionesha nia yake kwa Barca kutafuta suluhu la hali ya Olmo na Víctor haraka iwezekanavyo.

"Imesalia ladha mbaya kwa sababu ni wachezaji wenzetu," aliwaambia wanahabari. "Tunatumaini klabu inaweza kutatua suala hilo."

Araujo hakuwa amecheza tangu alipoumia msuli wa paja akiiwakilisha Uruguay kwenye Copa America Julai mwaka jana, lakini aliweza kukamilisha dakika 90 Jumamosi.

HABARI MICHEZO

# JKU SASA KUSHUSHA STRAIKA MPYA KUTOKA CAMEROON

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya JKU SC ipo mbioni kukamilisha usajili wa mchezaji kutoka nchini Cameroon katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili.

JKU SC ndio bingwa mtetezi wa Ligi Kuu Zanzibar, lakini imekuwa na mwanzo mbaya katika mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo yenye timu 16.

Katika michezo 14 iliyocheza, imefanikiwa kushinda mitano, sare sita na kupoteza mitatu, hivyo kushika nafasi ya tisa katika msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na alama 21.

Akizungumza na gazeti hili Katibu Mkuu wa timu hiyo, Shazil Khatib, alisema wapo katika hatua ya mwisho kukamilisha usajili wa mchezaji huyo ambaye wanaamini ataisaidia timu hiyo.

Alisema kamati ya usajili ya timu hiyo imemfuatili na imejiridhisha kuwa ana uwezo wa kujiunga katika kikosi chao.

"Tunaamini usajili tutakaoufanya utaweza kuziba mwanya ambao upo hivi sasa katika safu ya ushambuliaji, hivyo tumefikia sehemu kubwa ya mazungumzo tutakapomalizana naye basi tutaweka wazi kila kitu," alisema.

Aidha, alisema mbali na usajili huo kutoka nje ya Tanzania, lakini pia wanampango wa kusajili mchezaji mmoja kutoka Tanzania Bara ambapo pia wataweka wazi anatokea timu gani.

Alisema timu hiyo itasajili wachezaji watatu, lakini pia imepanga kuwapandisha daraja wachezaji wao watatu kutoka katika akademi yao.

Hata hivyo, alisema kama uongozi bado hawajakata tamaa ya kutetea ubingwa wao kwani wanayo nafasi ya kufanya hivyo kutokana utofauti mdogo wa alama katika msimamo wa ligi hiyo.

ISIWE TABU!...



Mchezaji wa Timu ya Mapinga Veteran, Bakula Mohamed (kulia), akimiliki mpira huku Levis Chilemeje wa Dar City, akijaribu kumthibiti wakati wa mechi ya kirafiki katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tabora United yafuata kipa Gabon

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tabora United ipo kwenye mazungumzo na golikipa wa Gabon, Jean Noel Amonone, kwa ajili ya kumsajili ili kuwaongezea nguvu makipa walioopo sasa, Haroun Mandanda na Hussein Masalanga.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo, zinasema kipa huyo wa zamani wa Amazulu ya Afrika Kusini na AS Arta Solar ya Djibouti, ambaye pia huwa anaitwa mara kwa mara kwenye kikosi cha timu ya taifa, kama mambo yataenda vizuri atawasili nchini kwa ajili ya kuidakia timu hiyo katika mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtoa taarifa huyo aliongeza kuwa bado wanaendelea kuimarisha kikosi kutokana na ripoti ya kocha Anicet Kiazayidi, ambaye amewataka kuongeza nguvu kikosini dirisha hili la usajili. „Kocha amesema anahitaji mshambuliaji mmoja, viungo watatu, beki mmoja na kipa na sisi tupo kwenye pilikapilika ya kuhakikisha tunapata watu ambao wataiwezesha timu kusonga mbele na kuendeleza heshima ambayo tayari imejipatia.

Ni kweli kuna changamoto kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, hakuna wachezaji wazuri sana kwa sababu wengi bado wana mikataba na klabu zao, vile vile hakuna timu ambayo wakati huu inaweza kumuachia mchezaji wake kwa urahisi kiasi hicho," kilisema chanzo chetu. Habari zinasema kipa huyo alimaliza mkataba wake na timu ya AS Arta Solar tangu Septemba 7, 2023 na baada ya hapo hakuwa na timu yoyote, hivyo Tabora United inakwenda kumsajili kama mchezaji huru.

Tabora United ambayo haikuanza vizuri sana Ligi Kuu msimu huu, imeonekana kuwa tishio baada ya ujio wa kocha Kiazayidi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akichukua nafasi ya Mkenya, Francis Kimanzi.

Hadi inamaliza mzunguko wa kwanza, inashika nafasi ya tano ikiwa na pointi 25 kwa michezo 15 iliyocheza, ikishinda saba, sare nne na kupoteza minne, ikifunga mabao 19 na kufungwa 19 pia.

## Ramovic: Hii ndiyo Yanga niliyoitaka

INATOKA UK. 24

tangu wakati tupo nyuma kwa bao moja, waliamini kuwa tutashinda mechi," alisema kocha huyo raia wa Ujerumani.

Alisema kwa jinsi timu zote mbili zilivyocheza, anadhani timu yake ilikuwa na uwezo wa kuondoka uwanjani ikiwa imefunga mabao saba au ikishinda 8-1.

"Nina uhakika kama tungekuwa makini tungeweza kuwafunga hata mabao saba au tungeshinda 8-1, tumekosa mabao mengi sana, lakini hiki tulichokipata tumefurahi, tumepambana na kujituma, kikosi kimeimarika sana," alisema.

Hata hivyo, alisema Kundi A, bado ni gumu na lipo wazi kwa timu yoyote kuweza kufuzu, hivyo kwa sasa wanajiandaa kwa michezo miwili waliyosalia nayo.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa TP Mazembe, Lamine Ndiaye, alilalamika kuwa bao la kwanza ambalo wapinzani walifunga lilikuwa la uonevu kwani, mchezaji wake alikuwa ameumizwa, hivyo mpira ulipaswa kutolewa nje, au mwamuzi kupiga filimbi.

"Mechi tumetizama wote, kipindi cha kwanza tuliikamata, tukapata nafasi, lakini hatukuzitumia. Goli la kwanza mchezaji wangu aliumia, badala ya mpira utolewe nje uliendelea tukafungwa bao la kusawazisha.

Goli la pili na la tatu, yalikuwa ni makosa ya wachezaji wangu wenyewe hawakuwa makini, nawapongeza Yanga, ni mpira," alisema kocha huyo raia wa Senegal.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Clement Mzize na moja la Stephane Aziz Ki, ambayo mbali na kuipa timu hiyo ushindi, yaliipandisha hadi nafasi ya tatu ya msimamo, ikifikisha jumla ya pointi nne, na kuivuta TP Mazembe mkiani, ikiwa na pointi mbili.

## Kiungo Simba atimkia Ulaya

INATOKA UK. 24

kiungo mshambuliaji, huku akisema hakuna haja ya kuongeza mshambuliaji wala winga katika kikosi chake kwa sasa.

„Nadhani baada ya mchezo dhidi ya CS Sfaxien, tutakaa na viongozi ili tuangalie ni nini tutafanya kwa ajili ya kuongeza wachezaji wachache kwenye kikosi," alisema.

Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu amethibitisha kuwa kwenye dirisha hili dogo la usajili klabu hiyo itatoa na kuingiza wachezaji kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi chao.

"Tuna utaratibu wetu, ni kweli tunahitaji marekebisho, tumeshaingia makubaliano ya klabu zingine kuhitaji wachezaji wao ili kuwasajili kwa ajili ya kutuongezea nguvu na kama tutawakosa tutakwenda sehemu nyingine, muda bado unatosha," alisema Mangungu.

# Michezo

Jumatatu Januari 6, 2025


Nipashe


## Arteta: Kamwe sijawahi kuona penalti kama hii

UKURASA 21



**SAMBARATISHA...**



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Stephane Aziz Ki, akiisambaratisha safu ya ulinzi ya TP Mazembe ya DR Congo, kwenye mechi ya Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na wenyeji kushinda mabao 3-1. **MPIGAPICHA WETU**

# Ramovic: Hii ndiyo Yanga niliyoitaka

Kasi, pumzi vyamkuna huku akisema aliona 8-1 dhidi ya TP Mazembe, lakini...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amekoshwa na kiwango cha wachezaji wake katika mchezo wa juzi wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, akisema hii ndiyo timu niliyokuwa „naitaka na kuihangaikia" tangu mwanzo, huku akiwaambia wapinzani wake kuwa wana bahati ya kutofungwa mabao saba au manane katika mchezo huo.

Akizungumza baada ya mchezo huo uliochezwa, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ikishinda mabao 3-1, Ramovic, alisema hiyo ndiyo Yanga aliyokuwa akiitaka tangu alipotua kwenye kikosi hicho na amekuwa akihangaika kuipata, lakini sasa anadhani imeshapatikana.

"Tumecheza na timu ngumu, tuliiheshimu kwa kile ambacho ilichofanya huko miaka ya nyuma, naipongeza kwa kutupa mechi ngumu. Tulihitaji pointi tatu kwa hali yoyote ili tuwe kwenye mbio za kufuzu hatua inayofuata.

Hiki sasa ndicho kiwango chetu, hii ndiyo Yanga niliyokuwa naitaka, wachezaji wangu wamejitahidi kuonesha kile ambacho tulichokuwa tukikihitaji hapo mwanzo wakati naingia kwenye timu hii.

Walikuwa na kasi, pumzi, walikaba na kutengeneza nafasi, hawakukata tamaa

INAENDELEA UK. 23

## Kiungo Simba atimkia Ulaya

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji aliyekuwa akifuatiliwa kwa karibu ili kujiunga na Klabu ya Simba kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili, Imourane Hassan, raia wa Benin, amerejea nchini Uswizi kujiunga na klabu yake mama ya Grasshopper Zurich, hivyo kuzima ndoto za Wekundu wa Msimbazi kumpata kipindi hiki.

Vyombo mbalimbali vya habari za michezo nchini Benin, vimeripoti kuwa kiungo huyo aliyekuwa akiichezea Loto Popo ya nchini kwao kwa mkopo kutoka Grasshopper, amerejeshwa kwenye timu hiyo huku mwenyewe akionekana kufurahishwa na hatua hiyo.

Habari zinasema kuwa kabla ya kurejea kwenye timu yake, Simba ilikuwa kwenye mazungumzo na mchezaji huyo akiwa na uwezo wa kucheza kiungo mkabaji na kiungo mshambuliaji pia.

Hata hivyo, magazeti kutoka Benin yanasema mbali na Simba ya Tanzania kumwania, Klabu ya Zamalek ya Misri nayo ilikuwa imeshatia mguu kutaka saini yake.

Uwezo alioonesha akiwa na Loto Popo ndio uliyoifanya timu yake iliyompeleka kwa mkopo kumrejesha tena kikosini na kuziacha kwenye nye mataa timu ambazo zilikuwa zikimtolea macho.

Hivi karibuni, chanzo kilisema tayari Simba ilikuwa imeanza mazungumzo na mchezaji huyo na yalikuwa yakiendelea vizuri.

Tukio hili limejirudia tena baada ya kumkosa Elie Mpanzu kutoka AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ambaye alikuwa asajiliwe na klabu hiyo mwanzoni mwa msimu huu, lakini ghafla alitimkia Genk ya Ubelgiji kwa ajili ya majaribio ambayo alifaulu tatizo likawa umri kwani kwa mujibu wa kanuni za mamlaka za soka za huko, kabla Wekundu wa Msimbazi kumnasa katika dirisha la usajili.

Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, alikiri kuwa kuna mapungufu kwenye baadhi ya maeneo na alitaka yaongezewe nguvu ikiwamo beki wa kati, kiungo mkabaji na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042